# Waamuzi

## *Waisraeli wapigana na Wakanaani waliobaki*

1 Baada ya kifo cha Yoshua, Waisraeli waka-
muuliza Mwenyezi Mungu, “Ni nani atakayetan-
gulia apande mbele yetu kutupigania dhidi ya
Wakanaani?”
2 Mwenyezi Mungu akajibu, “Yuda ndiye
atakayetangulia; nimewapa hiyo nchi mikononi
mwao.”
3 Ndipo wanaume wa Yuda wakawaambia
Wasimeoni ndugu zao, “Pandeni pamoja nasi
katika nchi tuliyopewa, ili tupate kupigana na
Wakanaani. Sisi pia tutaenda pamoja nanyi
katika sehemu yenu mliyopewa.” Basi Wasime-
oni wakaenda pamoja nao.
4 Yuda aliposhambulia, Mwenyezi Mungu
akawatia Wakanaani na Waperizi mikononi
mwao, nao wakawaua watu elfu kumi huko
Bezeki.
5 Huko ndiko walipomkuta huyo Adoni-
Bezeki, nao wakapigana naye na kuwafukuza
Wakanaani na Waperizi.
6 Adoni-Bezeki pia alikimbia, nao wakamfuata
na kumkamata, wakamkata vidole vyake gumba
vya mikono na vya miguu.
7 Ndipo Adoni-Bezeki akasema, “Wafalme
sabini waliokuwa wamekatwa vidole vyao
vya gumba vya mikono na vya miguu
walikuwa wakiokota makombo chini ya meza
yangu. Sasa Mungu amenilipa haya kwa yale

niliyowatendea.” Wakamleta Yerusalemu, naye
akafa huko.
8 Wanaume wa Yuda wakashambulia pia
Yerusalemu na kuiteka. Wakaupiga mji kwa
upanga na kuuchoma kwa moto.
9 Baada ya hayo, watu wa Yuda wakateremka
kupigana na Wakanaani walioishi katika nchi ya
vilima, na Negebu, na nchi ya Shefela*.
10 Yuda wakakabiliana na Wakanaani walioishi
Hebroni (mji huu hapo awali uliitwa Kiriath-Arba) na kuwashinda Sheshai, Ahimani na Talmai.
11 Kutoka huko wakasonga mbele kukabiliana
na watu walioishi Debiri (mji huu hapo awali
uliitwa Kiriath-Seferi).
12 Kalebu akasema, “Nitamwoza binti yangu
Aksa kwa mtu atakayepigana dhidi ya Kiriath-Seferi na kuuteka.”
13 Basi Othnieli mwana wa Kenazi, ndugu
mdogo wa huyo Kalebu, akawashinda; kwa hiyo
Kalebu akamtoa binti yake Aksa, akaolewa naye.
14 Siku moja Aksa alipokuja kwa Othnieli, alimsihi Othnieli amwombe baba yake, Kalebu,
shamba. Aksa aliposhuka kutoka punda wake,
Kalebu akamuuliza, “Je, wataka nikufanyie nini?”
15 Akamjibu, “Naomba unifanyie jambo moja la
hisani. Kwa kuwa umenipa ardhi huko Negebu,
nipe pia chemchemi za maji.” Ndipo Kalebu
akampa chemchemi za juu na za chini.
16 Wazao wa yule Mkeni, baba mkwe wa Musa,
wakapanda pamoja na watu wa Yuda kutoka Mji
wa Mitende†, wakaenda kuishi miongoni mwa

* **1:9** au *upande wa magharibi chini ya vilima* † **1:16** yaani *Yeriko*

watu wa jangwa la Yuda huko Negebu karibu na mji wa Aradi.

17 Basi wanaume wa Yuda wakaenda na Wasimeoni ndugu zao, wakawashambulia Wakanaani walioishi Sefathi, nao wakauangamiza huo mji kabisa. Kwa hiyo huo mji ukaitwa Horma‡.
18 Watu wa Yuda wakatwaa pia Gaza, Ashkeloni na Ekroni, kila mji na vijiji vyake vinavyouzunguka.

19 Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja na watu wa Yuda. Wakaimiliki nchi ya vilima, lakini hawakuweza kuwafukuza watu waliokaa katika hiyo tambarare, kwa sababu walikuwa na magari ya vita ya chuma.
20 Kama vile Musa alivyoahidi, Kalebu alipewa Hebroni, naye akawafukuza wana watatu wa Anaki.
21 Hata hivyo, Wabenyamini walishindwa kuwafukuza Wayebusi, walioishi Yerusalemu; hivyo hadi leo Wayebusi huishi humo pamoja na Wabenyamini.

22 Basi nyumba ya Yusufu wakashambulia Betheli, naye Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja nao.
23 Walipotuma watu kwenda kupeleleza Betheli (ambao hapo awali uliitwa Luzu),
24 wale wapelelezi wakaona mtu anatoka mjini, nao wakamwambia, “Tuoneshe jinsi ya kuingia mjini nasi tutakutendea wema.”

‡ **1:17** maana yake *Maangamizi*

25 Hivyo akawaonesha, nao wakaupiga mji kwa
upanga lakini wakamhifadhi hai yule mtu na
jamaa yake yote.
26 Yule mtu akaenda hadi nchi ya Wahiti, am-
bapo aliujenga mji na kuuita Luzu, ambalo ndilo
jina lake hadi leo.
27 Lakini Manase hawakuwafukuza watu wa
Beth-Shani na makazi yake, au watu wa Taanaki
na makazi yake, au watu wa Dori na makazi yake,
au watu wa Ibleamu na makazi yake, au watu wa
Megido na makazi yake, kwa kuwa Wakanaani
walikuwa wameamua kuishi katika nchi ile.
28 Israeli walipopata nguvu, wakawatia
Wakanaani katika kazi ya kulazimishwa, lakini
kamwe hawakuwafukuza watoke kabisa.
29 Wala Efraimu hawakuwafukuza kabisa
Wakanaani walioishi Gezeri, bali Wakanaani
waliendelea kuishi miongoni mwao.
30 Vivyo hivyo Zabuloni hawakuwafukuza
Wakanaani walioishi huko Kitroni, na walioishi
Nahaloli, bali Wakanaani hao walibaki miongoni
mwao; lakini waliwatia katika kazi ya kulaz-
imishwa.
31 Wala Asheri hawakuwafukuza wale
walioishi huko Ako, Sidoni, Alabu, Akzibu, Helba,
Afeki wala Rehobu,
32 na kwa sababu ya jambo hili Waasheri
wakaishi miongoni mwa Wakanaani, wenyeji wa
nchi.
33 Wala Naftali hawakuwafukuza wale
walioishi Beth-Shemeshi wala wale walioishi
Beth-Anathi; lakini Naftali nao pia wakaishi
miongoni mwa Wakanaani, wenyeji wa nchi,
nao wale walioishi Beth-Shemeshi na Beth-
Anathi wakawa watumishi wao katika kazi ya

kulazimishwa.
34 Waamori wakawazuilia Wadani kwenye
nchi ya vilima, na hawakuwaacha washuke kuin-
gia kwenye sehemu tambarare.
35 Waamori pia walikuwa wameamua kuen-
delea kuishi katika Mlima Heresi, Aiyaloni
na Shaalbimu; lakini nguvu ya nyumba ya
Yusufu ilipoongezeka, wao pia wakashindwa
na wakalazimika kuingia katika kazi ya kulaz-
imishwa.
36 Mpaka wa Waamori ulikuwa kuanzia Genge
la Akrabimu, kuendelea hadi Sela na kuelekea
juu.

# 2

## *Malaika wa Mwenyezi Mungu huko Bokimu*

1 Malaika wa Mwenyezi Mungu akakwea ku-
toka Gilgali hadi Bokimu, naye akasema, "Nili-
wapandisha kutoka Misri, na kuwaingiza katika
nchi niliyoapa kuwapa baba zenu. Nikasema,
'Kamwe sitalivunja agano langu nanyi.
2 Msifanye agano na watu wa nchi hii, bali
mtabomoa madhabahu yao.' Lakini ninyi
hamkunitii mimi. Kwa nini mmefanya jambo
hili?
3 Sasa basi ninawaambia kuwa sitawafukuza
watoke kati yenu, ila watakuwa mitego kwenu,
nayo miungu yao itakuwa tanzi kwenu."
4 Malaika wa Mwenyezi Mungu alipomaliza
kusema mambo haya kwa Waisraeli wote, watu
wakalia kwa sauti kuu.
5 Wakapaita mahali pale Bokimu. Nao wakam-
tolea Mwenyezi Mungu sadaka.

### *Kifo cha Yoshua*

6 Baada ya Yoshua kuwapa watu ruhusa
waende zao, Waisraeli wakaenda kwenye urithi
wao wenyewe ili kumiliki nchi yao.
7 Watu wakamtumikia Mwenyezi Mungu siku
zote za maisha ya Yoshua, na za hao wazee
walioishi baada ya Yoshua kufa, wale waliokuwa
wameona mambo makuu ambayo Mwenyezi
Mungu alikuwa ametenda kwa ajili ya Israeli.
8 Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa
Mwenyezi Mungu, akafa akiwa na umri wa mi-
aka mia moja na kumi.
9 Wakamzika katika nchi ya urithi wake,
huko Timnath-Heresi* katika nchi ya vilima ya
Efraimu, kaskazini mwa Mlima Gaashi.
10 Baada ya kizazi kile chote kukusanywa
pamoja na baba zao, kikainuka kizazi kingine
baada yao ambacho hakikumjua Mwenyezi
Mungu, wala matendo yale aliyokuwa ametenda
kwa ajili ya Waisraeli.
11 Kwa hiyo Waisraeli wakatenda maovu ma-
choni pa Mwenyezi Mungu na kuwatumikia
Mabaali.
12 Wakamwacha Mwenyezi Mungu, Mungu
wa baba zao, aliyekuwa amewatoa katika nchi
ya Misri. Wakaifuata na kuiabudu miungu
mbalimbali ya mataifa yaliyowazunguka.
Wakamkasirisha Mwenyezi Mungu,
13 kwa sababu walimwacha na kutumikia Baali
na Maashtorethi.

---

* **2:9** Unajulikana pia kama *Timnath-Sera*(taz. Yoshua 19:50; 24:30).

14 Hivyo hasira ya Mwenyezi Mungu ikawaka
juu ya Israeli, naye akawatia mikononi mwa
wavamizi waliowateka nyara. Akawauza
katika mikono ya adui zao pande zote, hivyo
hawakuweza tena kuwazuia adui zao.
15 Wakati wowote Israeli walipotoka kwenda
kupigana, mkono wa Mwenyezi Mungu
ulikuwa kinyume nao ili awashinde, kama vile
alivyokuwa amewaapia. Nao wakawa katika
taabu kubwa.

16 Ndipo Mwenyezi Mungu akawainua waa-
muzi, ambao waliwaokoa kutoka mikononi mwa
hao wavamizi.
17 Lakini hawakuwasikiliza hata waamuzi wao,
bali walifanya uasherati kwa kuifuata miungu
mingine na kuiabudu. Waligeuka upesi na
kuiacha njia ambayo baba zao waliiendea, yaani
njia ya kutii amri za Mwenyezi Mungu.
18 Kila mara Mwenyezi Mungu alipowainulia
mwamuzi, Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja
na huyo mwamuzi, naye aliwaokoa kutoka
mikononi mwa adui zao kwa kipindi chote ali-
choishi yule mwamuzi. Kwa kuwa Mwenyezi
Mungu aliwahurumia kwa sababu ya kilio chao
cha huzuni kwa ajili ya wale waliokuwa wakiwa-
tesa na kuwataabisha.
19 Lakini kila mara mwamuzi alipofariki, watu
walirudia katika hali mbaya ya uovu kuliko baba
zao, kwa kuifuata miungu mingine, ili kuitumikia
na kuiabudu. Walikataa kuacha matendo yao
maovu na njia zao za ukaidi.

20 Kwa hiyo Mwenyezi Mungu akawakasirikia
sana Israeli na kusema, “Kwa kuwa taifa hili

limevunja agano lile nililofanya na baba zao na hawakunisikiliza,
21 mimi nami sitafukuza taifa lolote ambalo Yoshua aliliacha alipofariki.
22 Nitawatumia mataifa hao ili nipate kuwapima Israeli, nione kama wataishika njia ya Mwenyezi Mungu na kuenenda kwa njia hiyo jinsi baba zao walivyofanya.”
23 Mwenyezi Mungu alikuwa ameyaacha hayo mataifa yabaki; hakuyaondoa mara moja kwa kuyatia mikononi mwa Yoshua.

# 3

## *Mataifa yaliyobaki katika nchi*

1 Haya ndio mataifa ambayo Mwenyezi Mungu aliyaacha ili kuwajaribu Waisraeli wote ambao hawakushiriki vita yoyote huko Kanaani
2 (alifanya hivi ili tu kuwafundisha vita wazao wa Waisraeli ambao hawakuwa na uzoefu wa vita hapo awali):
3 watawala watano wa Wafilisti, pamoja na Wakanaani wote, Wasidoni, na Wahivi walioishi katika milima ya Lebanoni kuanzia Mlima wa Baal-Hermoni hadi Lebo-Hamathi.
4 Waliachwa ili kuwajaribu Waisraeli, kuona kama wangetii amri za Mwenyezi Mungu, alizokuwa amewapa baba zao kwa mkono wa Musa.
5 Waisraeli wakaishi miongoni mwa Wakanaani, Wahiti, Waamori, Waperizi, Wahivi na Wayebusi.

6 Wakaoa binti za hao mataifa, na wakawatoa
binti zao wenyewe waolewe na wana wa hao
mataifa, na wakaitumikia miungu yao.

### *Othnieli*

7 Waisraeli wakafanya maovu machoni pa
Mwenyezi Mungu, wakamsahau Mwenyezi
Mungu, Mungu wao, na kutumikia Mabaali
na Maashera.
8 Hasira ya Mwenyezi Mungu ikawaka dhidi ya
Israeli. Hivyo akawauza mikononi mwa Kushan-
Rishathaimu mfalme wa Mesopotamia, nao Wais-
raeli wakamtumikia kwa muda wa miaka nane.
9 Waisraeli walipomlilia Mwenyezi Mungu,
yeye akawainulia mkombozi, Othnieli mwana
wa Kenazi, ndugu mdogo wa Kalebu, ambaye
aliwaokoa.
10 Roho wa Mwenyezi Mungu akaja juu yake;
hivyo akawa mwamuzi wa Israeli, na akaenda
vitani. Mwenyezi Mungu akamtia Kushan-
Rishathaimu mfalme wa Mesopotamia mikononi
mwa Othnieli, naye akamshinda.
11 Hivyo nchi ikawa na amani kwa muda wa
miaka arobaini, hadi Othnieli mwana wa Kenazi
alipofariki.

### *Ehudi*

12 Waisraeli wakafanya maovu mbele za
Mwenyezi Mungu tena; na kwa kuwa walifanya
maovu hayo, Mwenyezi Mungu akamtia nguvu
Egloni mfalme wa Moabu juu ya Israeli.
13 Egloni akawakusanya Waamoni na Waa-
maleki kwake, wakashambulia Israeli, na wakat-
waa Mji wa Mitende*.

---

* **3:13** yaani *Yeriko*

14 Waisraeli wakawa chini ya Egloni mfalme wa
Moabu kwa muda wa miaka kumi na nane.
15 Waisraeli wakamlilia tena Mwenyezi Mungu,
naye akawapa mkombozi: Ehudi, mtu wa shoto,
mwana wa Gera Mbenyamini. Waisraeli waka-
tuma kwa Egloni mfalme wa Moabu ushuru kwa
mkono wa Ehudi.
16 Basi Ehudi alikuwa ametengeneza upanga
ukatao kuwili, ukiwa na urefu wa kama dhi-
raa moja†, naye akaufunga upanga huo ndani
ya nguo yake, kwenye paja lake la mkono wa
kuume.
17 Akamkabidhi ushuru Egloni mfalme wa
Moabu, aliyekuwa mtu mnene sana.
18 Baada ya Ehudi kumkabidhi ule ushuru,
akawatuma wale watu waliokuwa wameubeba
huo ushuru waende zao.
19 Ehudi akafuatana nao hadi kwenye sanamu
za mawe karibu na Gilgali, ndipo yeye akarudi,
akafika kwa Egloni na kusema, “Ee Mfalme, ninao
ujumbe wa siri kwako.”

Mfalme akasema, “Nyamazeni kimya!” Nao wale waliomhudumia wote wakamwacha, wakatoka nje.

20 Ndipo Ehudi akamsogelea alipokuwa
ameketi peke yake kwenye chumba cha juu
cha jumba lake la kifalme la majira ya kiangazi,
na kusema, “Ninao ujumbe kutoka kwa Mungu
kwa ajili yako.” Mfalme alipokuwa anainuka
kutoka kiti chake,
21 Ehudi akaunyoosha mkono wake wa kushoto
na kuufuta ule upanga aliokuwa ameufunga

† **3:16** Dhiraa moja ni sawa na sentimita 45.

kwenye paja lake la kulia, akamdunga Mfalme
Egloni tumboni mwake.
22 Hata mpini nao ukazama tumboni pamoja
na upanga wenyewe, nao upanga ukatokea
mgongoni mwake. Ehudi hakuuchomoa huo
upanga, nayo mafuta yakashikamana juu ya up-
anga.
23 Ehudi akatoka nje barazani; akamfungia
milango ya chumba cha juu, na kuifunga kwa
funguo.
24 Baada yake kuondoka, watumishi wakaja na
kupata milango ya chumba cha juu imefungwa
kwa funguo. Wakasema, “Bila shaka anajisaidia
chumba cha ndani.”
25 Wakangoja hadi wakawa na fadhaa, na
wakati hakuifungua milango ya chumba,
wakachukua funguo na kuifungua. Tazama,
wakaona bwana wao amelala sakafuni, amekufa.
26 Walipokuwa wangali wanangoja, Ehudi aka-
toroka, akapita hapo kwenye sanamu ya kuchora
kwenye mawe na kukimbilia Seira.
27 Alipofika huko, akapiga tarumbeta katika
nchi ya vilima ya Efraimu, nao Waisraeli
wakateremka pamoja naye kutoka vilimani, yeye
akiwa anawaongoza.
28 Akawaagiza, “Nifuateni, kwa kuwa
Mwenyezi Mungu amewatia Moabu, adui zenu,
mikononi mwenu.” Kwa hiyo wakateremka
wakamfuata, wakavishika vivuko vya Yordani
kuelekea Moabu, wala hawakumwacha mtu
yeyote kuvuka.
29 Wakati huo wakawaua Wamoabu wapatao
elfu kumi wenye nguvu na mashujaa; hakuna

yeyote aliyetoroka.
30 Siku ile Moabu wakashindwa na Israeli, nayo
nchi ikawa na amani kwa miaka themanini.

### *Shamgari*

31 Baada ya Ehudi akaja Shamgari mwana wa
Anathi, aliyewapiga Wafilisti mia sita kwa fimbo
ya ng'ombe. Naye pia akawaokoa Waisraeli.

# 4

### *Debora*

1 Baada ya Ehudi kufa, Waisraeli wakafanya
tena maovu machoni pa Mwenyezi Mungu.
2 Hivyo Mwenyezi Mungu akawatia mikononi
mwa Yabini, mfalme wa Kanaani, aliyetawala
huko Hazori. Jemadari wa jeshi lake alikuwa
Sisera, aliyeishi huko Haroshethi-Hagoyimu*.
3 Kwa kuwa Sisera alikuwa na magari ya vita ya
chuma yapatayo mia tisa, naye alikuwa amewa-
tesa Waisraeli kwa ukatili kwa muda wa miaka
ishirini, Waisraeli wakamlilia Mwenyezi Mungu
wakaomba msaada.
4 Debora, nabii mwanamke, mkewe Lapidothi,
ndiye alikuwa anaamua Israeli wakati ule.
5 Debora alikuwa akiketi chini ya Mtende wa
Debora uliokuwa kati ya Rama na Betheli katika
nchi ya vilima ya Efraimu, nao Waisraeli wakaja
kwake ili awaamue.
6 Akatuma wamwite Baraka mwana wa
Abinoamu kutoka Kedeshi huko Naftali na
kumwambia, "Mwenyezi Mungu, Mungu wa
Israeli, anakuagiza: 'Nenda, chukua wanaume

---

* **4:2** yaani *Haroshethi ya Mataifa*

elfu kumi toka Naftali na Zabuloni, mwende
Mlima Tabori.
7 Nitamshawishi Sisera, jemadari wa jeshi la
Yabini, pamoja na magari yake ya vita na jeshi
lake, hadi Mto Kishoni na kumtia mikononi
mwako.' "

8 Baraka akamwambia, "Ukienda pamoja
nami nitaenda, lakini usipoenda pamoja nami,
sitaenda."

9 Debora akamwambia, "Hakika nitaenda
pamoja nawe, lakini njia unayoiendea haitakupa
heshima wewe, kwa kuwa Mwenyezi Mungu
atamtia Sisera mikononi mwa mwanamke."
Hivyo Debora akaenda pamoja na Baraka hadi
Kedeshi,
10 ambapo Baraka aliwaita Zabuloni na Naftali.
Watu elfu kumi wakamfuata Baraka, na Debora
pia akaenda naye.

11 Basi Heberi, Mkeni, alikuwa amejitenga na
Wakeni wale wengine, yaani wazao wa Hobabu,
mkwewe Musa, naye akapiga hema lake karibu
na ule mti mkubwa wa mwaloni ulio Saananimu,
karibu na Kedeshi.
12 Sisera alipoambiwa kuwa Baraka mwana wa
Abinoamu alikuwa amepanda Mlima Tabori,
13 Sisera akakusanya magari yake ya vita ya
chuma mia tisa, na watu wote waliokuwa pamoja
naye, kuanzia Haroshethi-Hagoyimu hadi Mto
wa Kishoni.
14 Ndipo Debora akamwambia Baraka, "Nenda!
Hii ndiyo siku ambayo Mwenyezi Mungu amem-
tia Sisera mikononi mwako. Je, Mwenyezi Mungu
hakukutangulia mbele yako?" Hivyo Baraka

akashuka kutoka Mlima Tabori, akifuatwa na watu elfu kumi.

15 Mwenyezi Mungu akamfadhaisha Sisera na
magari yake ya vita yote, pamoja na jeshi lake
lote kwa upanga mbele ya Baraka, naye Sisera
akaliacha gari lake la vita na kukimbia kwa
miguu.
16 Lakini Baraka akafuata magari ya vita
pamoja na jeshi hadi Haroshethi-Hagoyimu.
Jeshi lote la Sisera likaanguka kwa upanga, wala
hakuna hata mtu mmoja aliyesalia.

17 Sisera, hata hivyo, akakimbia kwa miguu
hadi kwenye hema la Yaeli, mkewe Heberi,
Mkeni, kwa sababu palikuwa na uhusiano wa
kirafiki kati ya Yabini mfalme wa Hazori na ukoo
wa Heberi, Mkeni.
18 Yaeli akaenda kumlaki Sisera na
kumwambia, "Karibu, bwana wangu, karibu
ingia ndani kabisa. Usiogope." Basi Sisera
akaingia ndani ya hema la Yaeli, naye
akamfunika kwa blanketi nene.
19 Akamwambia, "Nina kiu, tafadhali nipe maji
ya kunywa." Ndipo akafungua kiriba cha maziwa
na kumpa akanywa, kisha akamfunika.

20 Naye Sisera akamwambia, "Simama mlan-
goni pa hema na mtu yeyote akija na kukuuliza,
'Je, kuna mtu yeyote hapa?' sema, 'Hapana.' "

21 Lakini Yaeli, mkewe Heberi, akatwaa kigingi
cha hema, akachukua nyundo mkononi mwake,
akamwendea polepole, akiwa amelala usingizi
kwa kuchoka. Akakipigilia kile kigingi kwenye
paji la uso wake, kikapenya hata kuingia ardhini,
naye akafa.

22 Baraka akakaribia akimfuatia Sisera, Yaeli
akatoka kumlaki. Akamwambia, “Njoo, ni-
takuonesha mtu unayemtafuta.” Hivyo wakain-
gia ndani ya hema, na tazama, Sisera alikuwa
amelala humo akiwa amekufa, na hicho kigingi
cha hema kikiwa kimepigiliwa kupitia paji la uso
wake.
23 Basi siku ile Mungu akamshinda Yabini,
mfalme wa Kanaani, mbele ya Israeli.
24 Nao mkono wa Waisraeli ukaendelea kuwa
na nguvu zaidi na zaidi dhidi ya Yabini, mfalme
wa Kanaani, hadi wakamwangamiza.

# 5

*Wimbo wa Debora*

1 Siku hiyo Debora na Baraka mwana wa Abi-
noamu wakaimba wimbo huu:
2 “Wakuu katika Israeli wanapoongoza,
wakati watu wanapojitoa
kwa hiari yao wenyewe:
mhimidini Mwenyezi Mungu!

3 “Sikieni hili, enyi wafalme!
Sikilizeni, enyi watawala!
Nitamwimbia Mwenyezi Mungu, nitaimba;
kwa wimbo nitamhimidi Mwenyezi Mungu,
Mungu wa Israeli.

4 “Ee Mwenyezi Mungu, ulipotoka katika Seiri,
ulipopita katika mashamba ya Edomu,
nchi ilitetemeka, mbingu nazo zikamwaga,

naam, mawingu yakamwaga maji.
5 Milima ilitetemeka mbele za Mwenyezi Mungu,
Yule wa Sinai,
mbele za Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli.

6 “Katika siku za Shamgari mwana wa Anathi,
katika siku za Yaeli,
barabara kuu hazikuwa na watu;
wasafiri walipita njia za kando.
7 Mashujaa walikoma katika Israeli,
walikoma hadi mimi, Debora, nilipoinuka,
nilipoinuka kama mama katika Israeli.
8 Mungu alichagua viongozi wapya
vita vilipokuja malangoni ya mji;
lakini hapakuonekana ngao wala mkuki
miongoni mwa watu elfu arobaini katika Israeli.
9 Moyo wangu u pamoja na wakuu wa Israeli,
u pamoja na wale wanaojitoa kwa hiari yao
miongoni mwa watu.
Mhimidini Mwenyezi Mungu!

10 “Ninyi mpandao punda weupe,
mkiketi juu ya matandiko ya thamani,
nanyi mnaotembea barabarani,
fikirini
11 kuhusu sauti za waimbaji
mahali pa kunyweshea maji.
Wanasimulia matendo ya haki ya Mwenyezi Mungu,
matendo ya haki ya mashujaa wake
katika Israeli.

“Ndipo watu wa Mwenyezi Mungu
walipoteremka malangoni pa mji.
12 ‘Amka, amka! Debora!
Amka, amka, uimbe!
Ee Baraka! Inuka,
chukua mateka wako uliowateka,
ee mwana wa Abinoamu.’

13 “Ndipo mabaki ya watu
wakashuka dhidi ya wakuu,
watu wa Mwenyezi Mungu wakashuka kwangu
dhidi ya wenye nguvu.
14 Baadhi yao walitoka Efraimu,
ambao chimbuko lao ni Amaleki;
Benyamini alikuwa miongoni
mwa watu waliokufuata.
Kutoka Makiri wakashuka viongozi,
na kutoka Zabuloni wale washikao
fimbo ya jemadari.
15 Wakuu wa Isakari walikuwa pamoja na Debora;
naam, Isakari alikuwa pamoja na Baraka,
wakija nyuma yake kwa mbio
wakielekea bondeni.
Katika jamaa za Reubeni,
palikuwa na kujihoji kukubwa moyoni.
16 Kwa nini ulikaa katikati ya mazizi ya kondoo
kusikiliza sauti ya filimbi zinazoita makundi?
Kwa jamaa za Reubeni,
palikuwa na kujihoji kukubwa moyoni.
17 Gileadi alikaa ng’ambo ya Yordani.
Naye Dani, kwa nini alikaa
kwenye merikebu siku nyingi?

Asheri alikaa kwa utulivu ufuoni mwa bahari,
akikaa kwenye ghuba zake ndogo.
18 Watu wa Zabuloni walihatarisha maisha yao,
vilevile nao watu wa Naftali.

19 “Wafalme walikuja na kufanya vita;
wafalme wa Kanaani walipigana
huko Taanaki, karibu na maji ya Megido,
lakini hawakuchukua nyara za fedha.
20 Kutoka mbinguni nyota zilipigana,
nyota kutoka njia zake
zilipigana na Sisera.
21 Mto wa Kishoni uliwasomba,
ule mto wa zamani, mto wa Kishoni.
Songa mbele, ee nafsi yangu,
kwa ujasiri!
22 Ndipo kwato za farasi zikafanya mshindo:
farasi wake wenye nguvu
huenda mbio kwa kurukaruka.
23 Malaika wa Mwenyezi Mungu akasema, ‘Laani Merozi.
Laani watu wake kwa uchungu,
kwa kuwa hawakuja kumsaidia Mwenyezi Mungu,
kumsaidia Mwenyezi Mungu dhidi ya hao wenye nguvu.’

24 “Yaeli abarikiwe kuliko wanawake wote,
mkewe Heberi, Mkeni,
abarikiwe kuliko wanawake wote
wanaoishi kwenye mahema.
25 Sisera alimwomba maji, naye akampa maziwa;
kwenye bakuli la heshima

akamletea maziwa mgando.
26 Akanyoosha mkono wake
akashika kigingi cha hema,
mkono wake wa kuume
ukashika nyundo ya fundi.
Akampiga Sisera kwa nyundo,
akamponda kichwa chake,
akamvunjavunja na kumtoboa
paji lake la uso.
27 Aliinama miguuni pa Yaeli,
akaanguka; akalala hapo.
Alipoinama miguuni pake,
alianguka;
pale alipoinamia, ndipo alipoanguka,
akiwa amekufa.

28 “Kupitia dirishani mamaye Sisera alichungulia;
nyuma ya dirisha alilia, akasema,
‘Mbona gari lake la vita linachelewa kufika?
Mbona vishindo vya magari yake ya vita
vimechelewa?’
29 Wajakazi wale wenye busara
kuliko wengine wote wanamjibu;
naam, naye anasema moyoni mwake,
30 ‘Je, hawapati na kugawanya nyara:
msichana mmoja au wawili kwa kila mtu,
mavazi ya rangi mbalimbali kwa Sisera kuwa nyara,
mavazi ya rangi mbalimbali yaliyotariziwa,
mavazi yaliyotariziwa vizuri kwa ajili ya shingo yangu:
haya yote yakiwa nyara?’

31 “Adui zako wote na waangamie hivyo, Ee
Mwenyezi Mungu!
Bali wote wanaokupenda na wawe kama jua
linavyochomoza kwa nguvu zake.”

Hivyo nchi ikawa na amani kwa miaka arobaini.

# 6

*Gideoni*

1 Waisraeli wakafanya tena yaliyo maovu
mbele za Mwenyezi Mungu, naye Mwenyezi
Mungu akawatia mikononi mwa Wamidiani kwa
muda wa miaka saba.
2 Kwa kuwa Wamidiani walikuwa na nguvu
juu yao, Waisraeli walijitengenezea maficho mil-
imani, kwenye mapango, na katika ngome.
3 Kila wakati Waisraeli walipopanda mazao
mashambani, Wamidiani, Waamaleki na mataifa
mengine ya mashariki walivamia nchi yao.
4 Wakapiga kambi katika mashamba yao na
kuharibu mazao ya nchi yote hadi kufikia Gaza,
wala hawakuacha kiumbe chochote kilicho hai
kwa Waisraeli, iwe kondoo au ng'ombe au punda.
5 Walipanda na mifugo yao na mahema yao,
mfano wa makundi ya nzige. Ilikuwa hai-
wezekani kuwahesabu watu na ngamia wao;
wakavamia nchi ili kuiharibu.
6 Wamidiani wakaifanya Israeli kuwa mask-
ini sana, hata Waisraeli wakamlilia Mwenyezi
Mungu kumwomba msaada.
7 Waisraeli walipomlilia Mwenyezi Mungu kwa
sababu ya Wamidiani,

8 Mwenyezi Mungu akawapelekea nabii, ambaye aliwaambia, “Hili ndilo Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli, asemalo: Niliwapandisha mtoke Misri, toka nchi ya utumwa.
9 Nikawaokoa kutoka mikononi mwa Wamisri na kutoka mikononi mwa watesi wenu wote. Nikawafukuza watoke mbele yenu, nami nikawapa ninyi nchi yao.
10 Nikawaambia, ‘Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu; msiiabudu miungu ya Waamori, ambao mnakaa katika nchi yao!’ Lakini ninyi hamkuitii sauti yangu.”

11 Malaika wa Mwenyezi Mungu akaja akaketi chini ya mwaloni ulio Ofra, ambao ulikuwa mali ya Yoashi Mwabiezeri, pale Gideoni mwanawe alikuwa akipepeta ngano penye shinikizo la kukamulia zabibu, ili kuificha Wamidiani wasiione.
12 Malaika wa Mwenyezi Mungu alipomtokea Gideoni, akamwambia, “Mwenyezi Mungu yu pamoja nawe, ewe shujaa mwenye nguvu.”

13 Gideoni akajibu, “Nisamehe, Ee Bwana wangu. Kama Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametutokea? Yako wapi yale matendo yake makuu ambayo baba zetu walitusimulia juu yake waliposema, ‘Je, Mwenyezi Mungu hakutupandisha kutoka Misri?’ Lakini sasa Mwenyezi Mungu ametuacha na kututia katika mkono wa Midiani.”
14 Mwenyezi Mungu akamgeukia na kusema “Nenda kwa uwezo wako huu, ukawaokoe Israeli kutoka mikononi mwa Wamidiani. Je, si mimi ninayekutuma wewe?”

15 Gideoni akauliza, “Ee Bwana wangu,
nitawezaje kuwaokoa Israeli? Ukoo wangu ndio
dhaifu kuliko zote katika Manase, nami ndiye
mdogo wa wote katika jamaa yangu.”
16 Mwenyezi Mungu akamjibu, “Nitakuwa
pamoja nawe, nawe utawapiga Wamidiani kana
kwamba walikuwa ni mtu mmoja.”
17 Gideoni akajibu, “Kama basi nimepata kibali
machoni pako, nipe ishara kuonesha kuwa kweli
ni wewe unayesema nami.
18 Tafadhali nakuomba usiondoke hapa hadi
nitakaporudi, nilete sadaka yangu na kuiweka
mbele yako.”
Naye Mwenyezi Mungu akamwambia, “Nitangoja hadi utakaporudi.”
19 Gideoni akaingia ndani ya nyumba yake
na kuandaa mwana-mbuzi pamoja na kuoka
mikate isiyotiwa chachu kutokana na efa moja*
ya unga. Akaweka nyama kwenye kikapu na
mchuzi kwenye chungu, akamletea huyo malaika
hapo nje chini ya mwaloni, akampa.
20 Malaika wa Mungu akamwambia, “Itwae
nyama na mikate isiyotiwa chachu, uviweke juu
ya mwamba huu na umimine huo mchuzi juu
yake.” Gideoni akafanya hivyo.
21 Malaika wa Mwenyezi Mungu akainyoosha
fimbo iliyokuwa mkononi mwake, ncha yake
ikagusa ile nyama na ile mikate isiyotiwa chachu,
nao moto ukatoka kwenye mwamba ukateketeza
ile nyama na ile mikate. Malaika wa Mwenyezi
Mungu akatoweka machoni pake.

* **6:19** Efa moja ni sawa na lita 22.

22 Gideoni alipotambua kuwa ni malaika wa
Mwenyezi Mungu, akapaza sauti, akasema, "Ole
wangu, Bwana Mungu Mwenyezi! Kwa kuwa
nimemwona malaika wa Mwenyezi Mungu uso
kwa uso!"
23 Lakini Mwenyezi Mungu akamwambia,
"Amani iwe kwako! Usiogope. Hutakufa."

24 Hivyo Gideoni akamjengea Mwenyezi
Mungu madhabahu mahali pale na kupaita
Yehova-Shalomu†. Hata leo imesimama huko
Ofra ya Waabiezeri.

25 Usiku ule ule Mwenyezi Mungu
akamwambia, "Mchukue ng'ombe dume wa
baba yako, yule wa pili mwenye miaka saba,
ubomoe madhabahu ya Baali aliyo nayo baba
yako, na ukaikate nguzo ya Ashera iliyo karibu
nayo.
26 Kisha mjengee Mwenyezi Mungu, Mungu
wako, madhabahu kwa taratibu zake juu ya
mwamba katika ngome hii. Kwa kutumia kuni
za hiyo nguzo ya Ashera uliyoikatakata, mtoe
sadaka huyo dume wa pili kuwa sadaka ya
kuteketezwa."
27 Basi Gideoni akawachukua watumishi wake
kumi na kufanya kama Mwenyezi Mungu alivy-
omwambia. Lakini kwa kuwa aliwaogopa jamaa
yake na watu wa mji, akafanya haya usiku badala
ya mchana.

28 Watu wa mji walipoamka asubuhi, tazama
madhabahu ya Baali imebomolewa, na nguzo ya
Ashera iliyokuwa karibu nayo imekatwakatwa,

---

† **6:24** maana yake *Mwenyezi Mungu ni Amani*

na yule ng'ombe wa pili ametolewa sadaka juu ya madhabahu iliyojengwa upya!

29 Wakaulizana, "Ni nani aliyetenda mambo haya?"

Walipochunguza kwa makini, wakaambiwa, "Ni Gideoni mwana wa Yoashi, ndiye alitenda hivi."

30 Watu wa mji wakamwambia Yoashi, "Mlete
mwanao hapa. Ni lazima afe, kwa sababu amebomoa madhabahu ya Baali na kukatakata nguzo ya Ashera iliyokuwa karibu nayo."

31 Lakini Yoashi akaambia umati wa watu
waliomzunguka wakiwa kinyume naye, "Je, ninyi mtamtetea Baali? Mnajaribu kumwokoa? Yeyote mwenye kumpigania atauawa kufikia kesho asubuhi! Kama Baali ni mungu kweli, anaweza kujitetea mwenyewe wakati mtu anapobomoa madhabahu yake."

32 Basi siku ile wakamwita Gideoni "Yerub-
Baali," yaani "Baali na ashindane naye," kwa sababu alibomoa madhabahu yake.

33 Basi Wamidiani wote, Waamaleki na mataifa
mengine ya mashariki wakaunganisha majeshi yao, wakavuka ng'ambo ya Yordani na kupiga kambi katika Bonde la Yezreeli.
34 Ndipo Roho wa Mwenyezi Mungu akamjia
Gideoni, naye Gideoni akapiga tarumbeta kuwaita Waabiezeri ili wamfuate.
35 Akatuma wajumbe waende katika Manase
yote, akiwataka wachukue silaha na pia katika Asheri, Zabuloni na Naftali, nao wakakwea ili kukutana nao.

36 Gideoni akamwambia Mungu, “Kama
utawaokoa Waisraeli kwa mkono wangu, kama
ulivyoahidi:
37 tazama, nitaweka manyoya ya kondoo
kwenye sakafu ya kupuria nafaka, na kama
utakuwepo umande juu ya manyoya tu, na
ardhi yote ikiwa kavu, ndipo nitakapojua
kuwa utaokoa Israeli kwa mkono wangu, kama
ulivyosema.”
38 Hivyo ndivyo ilivyotokea. Gideoni akaamka
asubuhi na mapema kesho yake, akayakamua
yale manyoya yenye umande, yakatoka maji kiasi
cha kujaa bakuli.
39 Kisha Gideoni akamwambia Mwenyezi
Mungu, “Usinikasirikie. Ninaomba nifanye ombi
moja lingine. Niruhusu nifanye jaribio jingine
moja kwa manyoya haya. Wakati huu uyafanye
manyoya kuwa kavu, na ardhi yote ifunikwe na
umande.”
40 Usiku ule Mungu akafanya hivyo. Many-
oya yakawa kavu, na ardhi yote ikafunikwa na
umande.

# 7

### *Gideoni awashinda Wamidiani*

1 Ndipo Yerub-Baali (yaani Gideoni) na lile jeshi
lililokuwa pamoja naye, wakaondoka asubuhi
na mapema na kupiga kambi kando ya chem-
chemi ya Harodi. Kambi ya Wamidiani ilikuwa
kaskazini mwao katika bonde, karibu na kilima
cha More.
2 Mwenyezi Mungu akamwambia Gideoni,
“Jeshi lililo pamoja nawe ni kubwa sana kwangu

kuwatia Wamidiani mikononi mwao, Israeli asije akajisifu juu yangu, akisema, ‘Mkono wangu ndio uliniokoa.’
3 Kwa hiyo sasa tangaza jeshi lote likiwa linasikia, kwamba: ‘Yeyote anayeogopa na kutetemeka, yeye na arudi nyumbani, aondoke katika Mlima Gileadi.’ ” Hivyo, watu elfu ishirini na mbili wakarudi nyumbani, wakabaki elfu kumi.

4 Lakini Mwenyezi Mungu akamwambia Gideoni, “Idadi ya jeshi bado ni kubwa. Wapeleke kwenye maji, nami nitawajaribu huko kwa ajili yako. Nikikuambia, ‘Huyu ataenda pamoja nawe,’ yeye ataenda; lakini nikisema, ‘Huyu hataenda pamoja nawe,’ yeye hataenda.”

5 Gideoni akalipeleka lile jeshi kwenye maji, naye Mwenyezi Mungu akamwambia Gideoni, “Watenganishe watakaoramba maji kwa ulimi kama mbwa, na wale watakaopiga magoti ili kunywa.”
6 Waliokunywa kwa kuramba maji kutoka mikononi mwao walikuwa watu mia tatu. Wengine wote walipiga magoti ili kunywa.

7 Mwenyezi Mungu akamwambia Gideoni, “Kupitia hao watu mia tatu waliorambe maji nitawaokoa ninyi, nami nitawatia Wamidiani mkononi mwako. Waache hao watu wengine wote warudi kila mmoja nyumbani mwake.”
8 Hivyo Gideoni akawaruhusu wale Waisraeli wengine kila mmoja aende kwenye hema lake. Akabakia na wale mia tatu, nao wakachukua vyakula na tarumbeta za wenzao.

Basi kambi ya Wamidiani ilikuwa chini yake bondeni.
9 Usiku ule ule Mwenyezi Mungu akamwambia Gideoni, “Ondoka, ushuke ushambulie kambi, kwa kuwa nimeitia mkononi mwako.
10 Lakini kama unaogopa kushambulia, shuka kambini pamoja na mtumishi wako Pura,
11 nawe sikiliza wanayosema. Hatimaye, utatiwa moyo kushambulia kambi.” Basi yeye na Pura, mtumishi wake, wakashuka na kuwafikia walinzi wa mbele wa kambi.
12 Wamidiani, Waamaleki na mataifa mengine yote ya mashariki walikaa bondeni, nao walikuwa mfano wa nzige kwa wingi wao. Ngamia wao hawangehesabika, wingi wao ulikuwa kama mchanga wa ufuoni mwa bahari.
13 Gideoni alifika mara tu mtu mmoja alipokuwa akimweleza mwenzake ndoto yake, akisema, “Tazama, niliota ndoto, mkate wa shayiri uliovirингana ulianguka katika kambi ya Wamidiani, ukaipiga hema kwa nguvu, na kusababisha hema hilo kupinduka na kuporomoka.”
14 Rafiki yake akamjibu, “Habari hii si kitu kingine isipokuwa upanga wa Gideoni mwana wa Yoashi, Mwisraeli. Mungu amewatia Wamidiani na jeshi lote mkononi mwake.”
15 Gideoni alipoisikia hiyo ndoto na tafsiri yake, akasujudu na kuabudu. Akarudi kwenye kambi ya Israeli na kusema, “Inukeni! Mwenyezi Mungu amelitia jeshi la Wamidiani mikononi mwenu.”
16 Akawagawa wale watu mia tatu katika makundi matatu, akawakabidhi tarumbeta

mikononi mwao wote, na mitungi mitupu, na
mienge ikawekwa ndani yake.
17 Akawaambia, “Nitazameni, fanyeni kama
nitakavyofanya. Nitakapofika mwisho wa kambi,
mfanye kama nitakavyofanya.
18 Mimi na wote walio pamoja nami tu-
takapopiga tarumbeta zetu, ninyi nanyi pigeni
tarumbeta pande zote za kambi na mpige kelele,
mseme, ‘Upanga wa Mwenyezi Mungu na wa
Gideoni.’ ”
19 Gideoni na wale watu mia moja waliokuwa
pamoja naye wakafika mwisho wa kambi
usiku mwanzoni mwa zamu ya kati, mara tu
walipokuwa wamebadili zamu. Wakapiga zile
tarumbeta zao, na kuvunja ile mitungi iliyokuwa
mikononi mwao.
20 Yale makundi matatu wakapiga tarumbeta
na kuvunja mitungi. Wakashika mienge kwa
mikono yao ya kushoto, na tarumbeta katika
mikono yao ya kuume ili kuzipiga. Wakapaza
sauti zao, wakisema, “Upanga wa Mwenyezi
Mungu, na wa Gideoni!”
21 Wakasimama kila mtu mahali pake
kuizunguka kambi pande zote, Wamidiani wote
wakakimbia, huku wakipiga kelele.
22 Walipozipiga zile tarumbeta mia tatu,
Mwenyezi Mungu akafanya watu katika kambi
yote kugeukiana kila mmoja na mwenziwe
kwa upanga. Jeshi likakimbia hadi Beth-Shita
kuelekea Serera*, hadi mpakani mwa Abel-
Mehola karibu na Tabathi.

* **7:22** au *Seretha*

23 Wanaume Waisraeli wakaitwa kutoka Naf-
tali, Asheri na Manase yote, nao wakawafuatia
Wamidiani.
24 Gideoni akatuma wajumbe katika nchi yote
ya vilima ya Efraimu, akisema, “Teremkeni dhidi
ya Wamidiani na mkazuie vivuko vya maji mbele
yao hadi Beth-Bara na pia Yordani.”

Hivyo wanaume wote wa Efraimu wakakutanika pamoja na kuzingira vivuko vya maji mbele yao hadi Beth-Bara na pia Yordani.
25 Wakawakamata Orebu na Zeebu, wakuu
wawili wa Midiani. Wakamuua Orebu pale
penye mwamba wa Orebu, na Zeebu waka-
muua pale penye shinikizo la kukamulia zabibu
la Zeebu. Wakawafuatia Wamidiani na kuleta
vichwa vya Orebu na Zeebu kwa Gideoni, huko
ng’ambo ya Yordani.

# 8

*Ushindi wa Gideoni na kulipiza kisasi*

1 Basi Waefraimu wakamuuliza Gideoni,
“Mbona umetutenda hivi? Kwa nini
hukutuita ulipoenda kupigana na Wamidiani?”
Wakamlaumu kwa ukali sana.
2 Gideoni akawajibu, “Nilichofanya mimi ni
nini kulinganisha na kile ninyi mlichofanya? Je,
kuokoa masazo ya zabibu za Efraimu si bora
kuliko mavuno kamili ya zabibu ya Abiezeri?
3 Mungu amewatia Orebu na Zeebu, hao vion-
gozi wa Wamidiani, mikononi mwenu. Je,
mimi niliweza kufanya nini kulinganisha na mli-
chofanya ninyi?” Aliposema hili, hasira yao dhidi
yake ikatulia.

4 Gideoni pamoja na watu wake mia tatu,
wakiwa wamechoka sana lakini bado wakiwafu-
atia, wakafika Yordani na kuuvuka.
5 Akawaambia wanaume wa Sukothi, "Tafad-
hali lipatieni jeshi langu mikate, kwa maana
wamechoka, nami ningali ninawafuatia Zeba na
Salmuna, wafalme wa Midiani."

6 Lakini viongozi wa Sukothi wakasema, "Je,
tayari umewakamata Zeba na Salmuna ili tuli-
patie jeshi lako mikate?"

7 Gideoni akajibu, "Kwa ajili ya hilo tu,
Mwenyezi Mungu atakapowatia Zeba na
Salmuna mkononi mwangu, nitaichana nyama
ya miili yenu kwenye miiba ya nyikani na
kwenye michongoma."

8 Kutoka hapo alikwea hadi Penieli na ku-
toa ombi lile lile, lakini nao wanaume wa Pe-
nieli wakamjibu kama wanaume wa Sukothi
walivyokuwa wamemjibu.
9 Hivyo akawaambia wanaume wa Penieli,
"Nitakaporudi kwa ushindi, nitaubomoa mnara
huu."
10 Wakati huu Zeba na Salmuna walikuwa
Karkori, wakiwa na jeshi la watu wapatao elfu
kumi na tano waliokuwa wamesalia wa mataifa
ya mashariki, kwa kuwa watu wapatao elfu
mia moja na ishirini wenye panga walikuwa
wameuawa.
11 Basi Gideoni akakwea kwa njia ya wafugaji
wahamaji mashariki mwa Noba na Yogbeha, na
kulishambulia jeshi ambalo halikushuku lolote.
12 Zeba na Salmuna, hao wafalme wawili wa
Midiani, wakakimbia lakini yeye Gideoni akawa-

fuata na kuwakamata, akalishinda hilo jeshi lao lote kabisa.
13 Gideoni mwana wa Yoashi akarudi kutoka vitani kupitia Mwinuko wa Heresi.
14 Akamkamata kijana mmoja wa Sukothi na kumuuliza maswali, naye yule kijana akamwandikia majina ya viongozi sabini na saba wa Sukothi, ambao ni wazee wa mji.
15 Ndipo Gideoni akaja na kuwaambia wanaume wa Sukothi, "Tazameni Zeba na Salmuna mlionisimanga kwa ajili yao mkisema, 'Je, tayari umewakamata Zeba na Salmuna ili tulipatie jeshi lako mikate?' "
16 Akawachukua hao wazee wa mji, na kuwaadhibu wanaume wa Sukothi kwa kuwachapa kwa miiba na michongoma ya nyikani.
17 Pia akaubomoa mnara wa Penieli na kuwaua wanaume wa huo mji.
18 Kisha akawauliza Zeba na Salmuna, "Ni wanaume wa aina gani mliowaua huko Tabori?"

Wakajibu, "Ni wanaume kama wewe, kila mmoja wao akiwa anafanana na mwana wa mfalme."
19 Gideoni akajibu, "Hao walikuwa ndugu zangu, wana wa mama yangu hasa. Hakika kama Mwenyezi Mungu aishivyo, kama mngekuwa mmewaacha hai, mimi nisingewaua ninyi."
20 Akamgeukia Yetheri, mwanawe mzaliwa wa kwanza, akasema, "Waue hawa!" Lakini Yetheri hakuufuta upanga wake, kwa sababu aliogopa, kwa kuwa alikuwa bado kijana mdogo tu.
21 Zeba na Salmuna wakasema, "Njoo ufanye hivyo wewe mwenyewe. 'Alivyo mwanaume,

ndivyo zilivyo nguvu zake.' " Hivyo, Gideoni akajitokeza na kuwaua, naye akayaondoa mapambo kwenye shingo za ngamia wao.

### *Kizibau cha Gideoni*

22 Waisraeli wakamwambia Gideoni, "Ututawale, wewe, mwanao, na mjukuu wako, kwa kuwa umetuokoa kutoka mikononi mwa Wamidiani."
23 Lakini Gideoni akawaambia, "Mimi sitawatawala ninyi, wala mwanangu hatawatawala. Mwenyezi Mungu ndiye atakayewatawala ninyi."
24 Naye akasema, "Ninalo ombi moja, kwamba kila mmoja wenu anipatie kipuli kutoka fungu lake la nyara." (Ilikuwa desturi ya Waishmaeli kuvaa vipuli vya dhahabu.)
25 Wakajibu, "Tutafurahi kuvitoa." Hivyo wakatanda vazi chini na kila mwanaume akatupia juu yake pete kutoka fungu lake la nyara.
26 Uzito wa pete za dhahabu alizoomba ulikuwa shekeli elfu moja na mia saba*, bila kuhesabu mapambo mengine, vidani, na mavazi ya zambarau yaliyovaliwa na wafalme wa Midiani, au mikufu iliyokuwa kwenye shingo za ngamia wao.
27 Gideoni akatengeneza kizibau kwa kutumia ile dhahabu, ambacho alikiweka katika mji wake, yaani Ofra. Waisraeli wote wakafanya uasherati kwa kukiabudu huko, nacho kikawa mtego kwa Gideoni na jamaa yake.

* **8:26** Shekeli 1,700 ni sawa na kilo 19.5.

28 Hivyo Midiani wakashindwa mbele ya Waisraeli, nao hawakuinua vichwa vyao tena. Wakati wa siku za uhai wa Gideoni, nchi ikafurahia amani miaka arobaini.

### *Kifo cha Gideoni*

29 Yerub-Baali mwana wa Yoashi akarudi kwenda kuishi katika nyumba yake.
30 Alikuwa na wana sabini wa kwake mwenyewe, kwa kuwa alikuwa na wake wengi.
31 Suria wake, aliyekuwa anaishi huko Shekemu, pia alimzalia mwana, akamwita jina Abimeleki.
32 Gideoni mwana wa Yoashi akafa akiwa na umri mzuri wa uzee, akazikwa katika kaburi la Yoashi baba yake huko Ofra ya Waabiezeri.
33 Mara tu alipofariki Gideoni, Waisraeli wakarudia hali ya uovu na kufanya uasherati kwa kuabudu Mabaali. Wakamsimamisha Baal-Berithi kuwa mungu wao na
34 wala hawakumkumbuka Mwenyezi Mungu, Mungu wao, aliyewaokoa kutoka mikononi mwa adui zao wote kutoka kila upande.
35 Pia wakashindwa kuitendea mema jamaa ya Yerub-Baali (yaani Gideoni) kwa ajili ya mambo yote mema aliyokuwa amefanyia Israeli.

## 9

### *Abimeleki ajaribu kuanzisha ufalme*

1 Siku moja Abimeleki mwana wa Yerub-Baali akaenda kwa ndugu za mama yake huko Shekemu, akawaambia wao na ukoo wote wa mama yake,

2 “Waulizeni watu wote wa Shekemu, ‘Lipi lililo bora kwenu: Kutawaliwa na wana wote sabini wa Yerub-Baali, au mtu mmoja peke yake?’ Kumbukeni kwamba mimi ni mwili wenu na damu yenu.”

3 Ndugu za mama yake walipowaeleza watu wote wa Shekemu, wakaelekea kumkubali Abimeleki, kwa kuwa walisema, “Yeye ni ndugu yetu.”

4 Wakampa shekeli sabini* za fedha kutoka hekalu la Baal-Berithi, naye Abimeleki akazitumia kuajiri watu ovyo na wasiojali, wakawa ndio wafuasi wake.

5 Akaenda nyumbani mwa baba yake huko Ofra, na juu ya jiwe moja akawaua ndugu zake sabini, ambao ni wana wa Yerub-Baali. Lakini Yothamu, mwana mdogo kwa wote wa Yerub-Baali, akaokoka kwa kujificha.

6 Ndipo wenyeji wa Shekemu na Beth-Milo wakakusanyika pamoja chini ya mwaloni mkubwa, penye nguzo iliyo Shekemu, wakamtawaza Abimeleki kuwa mfalme.

7 Yothamu alipoambiwa hayo, akapanda juu ya kilele cha mlima Gerizimu, akapaza sauti, akawaambia, “Nisikilizeni enyi wenyeji wa Shekemu, ili Mungu naye apate kuwasikiliza.

8 Siku moja miti ilitoka ili kwenda kujitawazia mfalme. Ikauambia mzeituni, ‘Wewe uwe mfalme wetu.’

9 “Lakini mzeituni ukaijibu, ‘Je, niache kutoa mafuta yangu ambayo kwake miungu na wanadamu huheshimiwa, ili nikatawale miti?’

---

* **9:4** Shekeli 70 za fedha ni sawa na gramu 800.

10 “Kisha miti ikauambia mtini, ‘Njoo na uwe mfalme wetu!’

11 “Lakini mtini ukaijibu, ‘Je, niache kutoa matunda yangu mazuri na matamu, ili nikatawale miti?’

12 “Ndipo miti ikauambia mzabibu, ‘Njoo na uwe mfalme wetu.’

13 “Lakini mzabibu ukaijibu, ‘Je, niache kutoa divai yangu inayofurahisha miungu na wanadamu ili nikatawale miti?’

14 “Mwishoni miti yote ikauambia mchongoma, ‘Njoo na uwe mfalme wetu.’

15 “Nao mchongoma ukaijibu, ‘Kama kweli mnataka kunitawaza niwe mfalme wenu, basi njooni mpate kupumzika chini ya kivuli changu. Lakini kama sivyo, moto na utoke kwenye mchongoma ukateketeze mierezi ya Lebanoni!’

16 “Basi, je, mmetenda kwa uaminifu na heshima kwa kumtawaza Abimeleki kuwa mfalme? Je, mmetendea mema Yerub-Baali na jamaa yake, na mkamtendea kama alivyostahili?

17 Baba yangu aliwapigania na kuhatarisha nafsi yake ili kuwaokoa kutoka mikononi mwa Wamidiani,

18 lakini leo mmeasi dhidi ya jamaa ya baba yangu, na kuwaua wanawe sabini juu ya jiwe moja. Nanyi mmemtawaza Abimeleki mwana wa mjakazi wake kuwa mfalme juu ya wenyeji wa Shekemu, kwa kuwa yeye ni ndugu yenu.

19 Ikiwa kweli mmemtendea Yerub-Baali na jamaa yake kwa heshima na uaminifu, basi Abimeleki na awe furaha yenu, nanyi mwe furaha yake pia!

20 Lakini kama sivyo, moto na utoke kwa
Abimeleki na uwateketeze, ninyi wenyeji
wa Shekemu na Beth-Milo; nao moto utoke
kwenu, wenyeji wa Shekemu na Beth-Milo, na
umteketeze Abimeleki!”
21 Ndipo Yothamu akakimbia, akatoroka
akaenda Beeri, akaishi huko, kwa sababu
alimwogopa ndugu yake Abimeleki.

22 Baada ya Abimeleki kutawala Israeli kwa
muda wa miaka mitatu,
23 Mungu akaruhusu roho mbaya kati ya
Abimeleki na wenyeji wa Shekemu, nao wenyeji
wa Shekemu wakamtendea Abimeleki kwa hila.
24 Hili lilitendeka ili ule ukatili waliotendewa
hao wana sabini wa Yerub-Baali upatilizwe, na
damu yao iwe juu ya Abimeleki ndugu yao aliye-
waua, na pia iwe juu ya wenyeji wa Shekemu,
ambao walimsaidia kuua ndugu zake.
25 Hivyo, kutokana na uadui juu yake, wenyeji
wa Shekemu wakaweka watu wa kumvizia
katika vilele vya milima. Wakawanyang'anya
watu wote waliopita karibu nao, nayo haya
yakaarifiwa kwa Abimeleki.
26 Basi Gaali mwana wa Ebedi akaenda pamoja
na ndugu zake wakaingia Shekemu, nao wenyeji
wa huko wakawa na imani naye.
27 Wakaenda mashambani mwao kuvuna
zabibu na kuzisindika hizo zabibu, baadaye
wakafanya sherehe katika hekalu la mungu wao.
Walipokuwa wakila na kunywa, wakamlaani
Abimeleki.
28 Gaali mwana wa Ebedi akasema, “Abimeleki
ni nani, na Shekemu ni nani, hata tumtumikie?
Je, yeye si mwana wa Yerub-Baali? Naye Zebuli si

ndiye msaidizi wake? Basi watumikieni watu wa
Hamori, babaye Shekemu. Kwa nini tumtumikie
Abimeleki?
29 Laiti watu hawa wangekuwa chini ya
amri yangu! Basi mimi ningemwondoa huyo
Abimeleki. Ningemwambia Abimeleki, 'Ondoa
jeshi lako lote.' "

30 Zebuli aliyekuwa mtawala wa mji aliposikia
aliyosema Gaali mwana wa Ebedi, akakasirika
sana.
31 Akatuma wajumbe waende kwa Abimeleki
kwa siri, na kusema, "Gaali mwana wa Ebedi
na ndugu zake wamekuja Shekemu, na wanau-
chochea mji huu kinyume chako.
32 Sasa basi, usiku huu wewe uondoke na watu
wako ili mje kuwavizia mashambani.
33 Kisha asubuhi wakati wa kuchomoza jua,
amka mapema na ujipange dhidi ya huo mji.
Gaali na jeshi lililo pamoja naye watakapotoka
kukabiliana nanyi, mwaweza kuwatendea kwa
kadiri mnavyoweza."

34 Kwa hiyo Abimeleki pamoja na jeshi lake
lote wakaondoka usiku na kujificha karibu na
Shekemu wakiwa vikosi vinne.
35 Basi Gaali mwana wa Ebedi alikuwa ame-
toka nje akawa amesimama katika ingilio la mji
wakati ule ule ambao Abimeleki na watu wake
walipokuwa wanatoka sehemu zao za maficho.

36 Gaali alipowaona, akamwambia Zebuli,
"Tazama, watu wanashuka kutoka vilele vya mil-
ima!"

Zebuli akajibu, "Wewe unaona vivuli vya mil-
ima kana kwamba ni watu."

37 Lakini Gaali akasema tena, “Tazama, watu
wanashuka kutoka katikati ya nchi na kikosi
kimoja kinakuja kutoka Tabur-Ezeri na kikosi
kingine kutoka upande wa mwaloni wa Meonen-
imu.”
38 Ndipo Zebuli akamwambia, “Kuko wapi
kujivuna kwako sasa, wewe uliyesema, ‘Huyo
Abimeleki ni nani hata tumtumikie?’ Hawa si
wale watu uliowadharau? Toka nje sasa ukapi-
gane nao!”
39 Basi Gaali akawaongoza wenyeji wa
Shekemu kupigana na Abimeleki.
40 Abimeleki akamfukuza, naye akatoroka.
Nao watu wengi wakaanguka njia yote hadi
kwenye ingilio la lango, wakiwa wamejeruhiwa
katika kule kutoroka.
41 Abimeleki akaishi Aruma, naye Zebuli
akawafukuza Gaali na ndugu zake watoke
Shekemu.
42 Kesho yake watu wa Shekemu wakatoka
wakaenda mashambani, Abimeleki akaambiwa
jambo hilo.
43 Hivyo akawachukua watu wake, akawa-
gawanya katika vikosi vitatu na kuwaweka wav-
iziaji huko mashambani. Alipowaona watu
wanatoka kwenda nje ya mji, akainuka dhidi yao
na kuwashambulia.
44 Abimeleki pamoja na vikosi vyake
wakaharakisha kwenda mbele kwenye nafasi
iliyokuwa katika ingilio la lango la mji. Vikosi
viwili vikawashambulia wale waliokuwa
mashambani, na kuwaua.
45 Siku hiyo nzima Abimeleki akazidisha
mashambulizi yake dhidi ya mji hadi akawa

ameuteka na kuwaua watu wa mji huo. Kisha akauangamiza mji na kusambaza chumvi juu yake.

46 Kwa kusikia jambo hilo, watu wote katika mnara wa Shekemu wakaingia kwenye ngome ya hekalu la El-Berithi.
47 Abimeleki aliposikia kuwa wamekusanyika huko,
48 yeye na watu wake wote wakakwea kwenye Mlima Salmoni. Abimeleki akachukua shoka, akakata baadhi ya matawi, ambayo aliyachukua begani mwake. Akawaagiza wale watu waliokuwa pamoja naye kuwa, "Haraka! Fanyeni kile mmeona nikifanya!"
49 Basi watu wote wakakata matawi na kumfuata Abimeleki. Wakayakusanya hayo matawi juu ya ngome, na kuitia moto ili kuwachoma watu wote waliokuwa ndani. Hivyo watu wote katika mnara wa Shekemu, yamkini wanaume na wanawake elfu moja, pia wakafa.

50 Baadaye Abimeleki akaenda Thebesi na kuuzingira kwa jeshi na kuuteka.
51 Hata hivyo, ndani ya huo mji kulikuwa na mnara imara, ambako watu wote wa mji, wanaume na wanawake, walikimbilia ndani yake. Wakajifungia ndani, na kupanda juu ya paa la mnara.
52 Abimeleki akaja kwenye ule mnara na kushambulia. Lakini alipokaribia kwenye ingilio la mnara ili kuuchoma kwa moto,
53 mwanamke mmoja akaangusha sehemu ya juu ya jiwe la kusagia kwa kichwa cha Abimeleki, likapasua fuvu la kichwa chake.

54 Akamwita kwa haraka kijana yule
aliyechukua silaha zake, na kumwambia,
“Chukua upanga wako na uniue, watu wasije
wakasema, ‘Mwanamke amemuua.’ ” Basi yule
kijana akamchoma upanga, naye akafa.
55 Waisraeli walipoona kuwa Abimeleki amek-
ufa, kila mtu akaenda nyumbani mwake.
56 Hivyo ndivyo Mungu alivyolipiza uovu ule
ambao Abimeleki alikuwa ameutenda kwa baba
yake kwa kuwaua ndugu zake sabini.
57 Mungu akawapatiliza wanaume wa
Shekemu uovu wao juu ya vichwa vyao, na
juu yao ikaja laana ya Yothamu mwana wa
Yerub-Baali.

# 10

*Tola*

1 Baada ya Abimeleki, Tola mwana wa Pua
mwana wa Dodo, mtu wa Isakari, aliyeishi
huko Shamiri, katika nchi ya vilima ya Efraimu,
akainuka kuokoa Israeli.
2 Akawa mwamuzi wa Israeli kwa miaka
ishirini na tatu. Ndipo akafa, naye akazikwa
huko Shamiri.

*Yairi*

3 Baada yake akafuatiwa na Yairi, Mgileadi,
aliyekuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka
ishirini na mbili.
4 Alikuwa na wana thelathini waliopanda
punda thelathini. Nao walikuwa na miji the-
lathini huko Gileadi, inayoitwa Hawoth-Yairi
hadi leo.
5 Yairi akafa, naye akazikwa huko Kamoni.

### *Yefta*

6 Tena Waisraeli wakatenda maovu machoni
pa Mwenyezi Mungu. Wakaabudu Mabaali na
Maashtorethi, na miungu ya Aramu, miungu ya
Sidoni, miungu ya Moabu, miungu ya Waamoni,
na miungu ya Wafilisti. Na kwa kuwa Waisraeli
walimwacha Mwenyezi Mungu wala hawakuen-
delea kumtumikia,
7 hivyo hasira ya Mwenyezi Mungu ikawaka
dhidi ya Waisraeli. Naye akawatia mikononi
mwa Wafilisti na Waamoni,
8 ambao waliowaonea na kuwatesa mwaka
huo. Kwa miaka kumi na nane wakawatesa
Waisraeli wote upande wa mashariki mwa Mto
Yordani huko Gileadi, katika nchi ya Waamori.
9 Waamoni nao wakavuka Yordani ili kupigana
na Yuda, Benyamini na nyumba ya Efraimu, nayo
nyumba ya Israeli ikawa katika taabu kubwa.
10 Ndipo Waisraeli wakamlilia Mwenyezi
Mungu wakasema, “Tumetenda dhambi dhidi
yako, kumwacha Mungu wetu na kutumikia
Mabaali.”
11 Mwenyezi Mungu akawaambia, “Wamisri,
Waamori, Waamoni, Wafilisti,
12 Wasidoni, Waamaleki na Wamaoni
walipowadhulumu ninyi, nanyi mkanililia na
kuomba msaada, je, sikuwaokoa mikononi
mwao?
13 Lakini ninyi mmeniacha na kuitumikia mi-
ungu mingine, kwa hiyo sitawaokoa tena.
14 Nendeni mkaililie ile miungu mlioichagua.
Hiyo miungu na iwaokoe mnapokuwa katika
taabu!”

15 Lakini Waisraeli wakamwambia Mwenyezi
Mungu, “Tumetenda dhambi. Ututendee lile
unaloona kuwa jema kwako, lakini twakusihi
utuokoe sasa.”
16 Nao wakaiondoa hiyo miungu migeni kati
yao nao wakamtumikia Mwenyezi Mungu. Naye
akahuzunika kwa sababu ya taabu ya Israeli.
17 Waamoni walipoitwa vitani na kupiga kambi
kule Gileadi, Waisraeli walikusanyika na kupiga
kambi huko Mispa.
18 Viongozi wa watu wa Gileadi wakaambiana
wao kwa wao, “Yeyote atakayeanzisha masham-
bulizi dhidi ya Waamoni atakuwa kiongozi wa
wote wanaoishi Gileadi.”

# 11

1 Basi Yefta Mgileadi alikuwa shujaa mwenye
nguvu. Baba yake alikuwa Gileadi, naye mama
yake alikuwa kahaba.
2 Mke wa Gileadi pia akamzalia wana, nao
walipokua, wakamfukuza Yefta, na kumwambia,
“Wewe huwezi kupata urithi katika jamii yetu,
kwa sababu wewe ni mwana wa mwanamke
mwingine.”
3 Basi Yefta akawakimbia ndugu zake akaenda
kuishi katika nchi ya Tobu, mahali ambako watu
waasi walijiunga naye na kumfuata.
4 Baada ya muda Waamoni wakafanya vita na
Israeli,
5 viongozi wa Gileadi wakaenda kumchukua
Yefta katika nchi ya Tobu.
6 Wakamwambia Yefta, “Njoo, uwe jemadari
wetu, ili tuweze kupigana na Waamoni.”

7 Yefta akawaambia viongozi wa Gileadi, “Je,
si mlinichukia na kunifukuza nitoke katika
nyumba ya baba yangu? Kwa nini mwanijia sasa,
wakati mko taabuni?”
8 Viongozi wa Gileadi wakamwambia Yefta,
“Lakini sasa tumegeuka kukuelekea wewe, ili
uende pamoja nasi kupigana na Waamoni, nawe
utakuwa kiongozi wetu juu ya watu wote wa
Gileadi.”
9 Yefta akawaambia viongozi wa Gileadi, “Ikiwa
mtanirudisha kwetu kupigana na Waamoni, naye
Mwenyezi Mungu akanisaidia kuwashinda, je, ni
kweli nitakuwa kiongozi wenu?”
10 Viongozi wa Gileadi wakamjibu Yefta,
“Mwenyezi Mungu ndiye shahidi wetu. Kwa
hakika tutafanya kama usemavyo.”
11 Basi Yefta akaenda na viongozi wa Gileadi,
nao watu wakamfanya kiongozi na jemadari
wao. Naye akarudia maneno yake yote mbele za
Mwenyezi Mungu huko Mispa.
12 Ndipo Yefta akatuma wajumbe kwa mfalme
wa Waamoni akisema, “Una nini nasi, hata
umekuja kushambulia nchi yetu?”
13 Mfalme wa Waamoni akawajibu wajumbe
wale wa Yefta, “Waisraeli walipopanda kutoka
Misri, waliichukua nchi yangu kuanzia Mto
Arnoni hadi Mto Yaboki, hadi kufikia Mto Yor-
dani. Sasa irudishe kwa amani.”
14 Yefta akarudisha wajumbe kwa mfalme wa
Waamoni,
15 kusema:

“Hili ndilo asemalo Yefta: Waisraeli hawakuchukua nchi ya Moabu wala nchi ya Waamoni.

16 Lakini walipopanda kutoka Misri, Waisraeli walipitia katika jangwa hadi Bahari ya Shamu na wakafika Kadeshi.

17 Ndipo Waisraeli wakatuma wajumbe kwa mfalme wa Edomu, wakisema, 'Tupe ruhusa kupita katika nchi yako.' Lakini mfalme wa Edomu hakutusikia. Wakatuma wajumbe pia kwa mfalme wa Moabu, naye akakataa. Kwa hiyo Waisraeli wakakaa huko Kadeshi.

18 "Baadaye wakasafiri kupitia jangwa, wakiambaa na nchi za Edomu na Moabu, wakapitia upande wa mashariki wa nchi ya Moabu, na kupiga kambi upande ule mwingine wa Mto Arnoni. Hawakuingia katika nchi ya Moabu, kwa kuwa Mto Arnoni ulikuwa mpaka wake.

19 "Kisha Waisraeli wakatuma wajumbe kwa Sihoni mfalme wa Waamori, aliyetawala Heshboni, na kumwambia, 'Tupe ruhusa kupita katika nchi yako ili kufikia mahali petu.'

20 Hata hivyo, Sihoni hakuwaamini Waisraeli kupita katika nchi yake. Akaandaa jeshi lake lote na kupiga kambi huko Yahasa, nao wakapigana na Waisraeli.

21 "Ndipo Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli, akamtia Sihoni na watu wake wote mikononi mwa Waisraeli, nao wakawashinda. Waisraeli wakaimiliki nchi yote ya Waamori walioishi nchi hiyo,

22 wakiiteka nchi yote kuanzia Mto Arnoni hadi Mto Yaboki, na kutoka jangwani hadi Mto Yordani.

23 "Basi kwa kuwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli, amewafukuza Waamori watoke

mbele ya watu wake Israeli, wewe unayo haki gani ya kuitamalaki?

24 Je, haikupasi kuchukua kile ambacho mungu wako Kemoshi amekupa? Vivyo hivyo, chochote kile Mwenyezi Mungu, Mungu wetu, alichotupatia sisi, tutakimiliki.

25 Je, wewe ni bora kuliko Balaki mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu? Je, yeye alishagombana na Waisraeli au kupigana nao wakati wowote?

26 Kwa maana kwa miaka mia tatu, Waisraeli wameishi Heshboni na makazi yake, Aroeri na makazi yake, na katika miji yote iliyo kando ya Mto Arnoni. Kwa nini wewe hukuyachukua wakati huo?

27 Mimi sijakukosea, bali wewe ndiwe unanikosea kwa kufanya vita nami. Basi Mwenyezi Mungu, aliye Mwamuzi, leo na aamue ugomvi kati ya Waisraeli na Waamoni."

28 Hata hivyo, mfalme wa Waamoni hakuyajali maneno ya ujumbe wa Yefta.

29 Ndipo Roho wa Mwenyezi Mungu akaja juu ya Yefta. Akapita katikati ya Gileadi na Manase, pia akapita katika Mispa ya Gileadi, na kutokea huko akasonga mbele kushambulia Waamoni.

30 Naye Yefta akaweka nadhiri mbele za Mwenyezi Mungu akisema, "Ikiwa utawatia Waamoni mikononi mwangu,

31 chochote kile kitakachotoka katika mlango wa nyumba yangu cha kwanza ili kunilaki nirudipo kwa amani katika kuwashinda Waamoni, kitakuwa ni cha Mwenyezi Mungu na nitakitoa kuwa sadaka ya kuteketezwa."

32 Ndipo Yefta akavuka kupigana na hao Waamoni, naye Mwenyezi Mungu akawatia mkononi mwake.

33 Akaharibu kabisa miji ishirini kuanzia Aroeri hadi karibu na Minithi, na kuendelea hadi Abel-Keramimu. Hivyo, Waisraeli wakawashinda Waamoni.

34 Yefta aliporudi nyumbani mwake huko Mispa, tazama, binti yake akatoka ili kumlaki kwa matari na kucheza. Alikuwa mwanawe wa pekee, hakuwa na mwana wala binti mwingine.

35 Alipomwona akararua mavazi yake akalia, “Ee! Binti yangu! Umenifanya niwe na huzuni na kunyong’onyea sana, kwa kuwa nimeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu, ambayo siwezi kuivunja.”

36 Akajibu, “Baba yangu, umetoa neno lako kwa Mwenyezi Mungu. Nitendee mimi kama vile ulivyoahidi, kwa kuwa Mwenyezi Mungu amekupa ushindi dhidi ya adui zako Waamoni.”

37 Naye akamwambia baba yake, “Naomba nifanyiwe jambo hili. Nipewe miezi miwili ili kuzunguka vilimani nikaulilie ubikira wangu, mimi na wenzangu.”

38 Baba yake akamwambia, “Unaweza kwenda.” Naye akamwacha aende kwa miezi miwili. Hivyo akaondoka pamoja na wenzake, naye akaulilia ubikira wake huko vilimani kwa sababu hangeolewa kamwe.

39 Baada ya hiyo miezi miwili, alirejea kwa baba yake, naye baba yake akamtendea kama alivyokuwa ametoa nadhiri yake. Naye alikuwa bikira.

Nayo ikawa desturi katika Israeli,
40 kwamba kila mwaka binti za Israeli huenda
kwa siku nne ili kumkumbuka huyo binti Yefta
Mgileadi.

# 12

## *Yefta na Efraimu*

1 Watu wa Efraimu wakaita majeshi yao,
wakavuka kwenda Zafoni. Wakamwambia Yefta,
“Kwa nini mmeenda kupigana na Waamoni bila
kutuita ili twende pamoja nawe? Basi tutai-
choma moto nyumba yako, pamoja nawe ukiwa
ndani yake.”
2 Yefta akajibu, “Mimi na watu wangu tulikuwa
na ugomvi mkubwa na Waamoni. Ingawa nili-
waita, hamkuniokoa kutoka mkono wao.
3 Nilipoona kuwa hamniokoi, nikauhatarisha
uhai wangu, nikavuka kupigana na Waamoni.
Naye Mwenyezi Mungu akanipatia ushindi dhidi
yao. Sasa kwa nini mnanijia leo ili kupigana
nami?”
4 Ndipo Yefta akakusanya wanaume wa Gileadi
pamoja na kupigana na Efraimu. Wagileadi
wakawashinda Waefraimu, kwa kuwa Wae-
fraimu walisema, “Ninyi Wagileadi ni waasi
mliotoroka toka Efraimu na Manase.”
5 Wagileadi wakaviteka vivuko vya Mto Yor-
dani kuelekea Efraimu. Kisha ilikuwa yeyote
aliyenusurika kutoka Efraimu aliposema, “Ni-
ache nivuke,” hao wanaume wa Gileadi wal-
imuuliza, “Je wewe ni Mwefraimu?” Akijibu
“Hapana,”

6 walimwambia, “Sawa, sema ‘Shibolethi’.” Iwapo alitamka, “Sibolethi”, kwa sababu hakuweza kutamka hilo neno sawasawa, walimkamata na kumuua hapo kwenye vivuko vya Mto Yordani. Waefraimu elfu arobaini na mbili waliuawa wakati huo.

7 Yefta akawa mwamuzi wa Waisraeli kwa muda wa miaka sita. Kisha Yefta akafa, akazikwa katika mmoja wa miji ya Gileadi.

### *Ibzani, Eloni na Abdoni*

8 Baada yake, Ibzani wa Bethlehemu akawa mwamuzi wa Israeli.
9 Alikuwa na wana thelathini na binti thelathini. Akawaoza binti zake kwa watu wengine nje ya ukoo wake, na kuwatwalia wanawe wanawake thelathini toka nje ya ukoo wake. Ibzani akawa mwamuzi wa Israeli kwa muda wa miaka saba.
10 Kisha Ibzani akafa, akazikwa huko Bethlehemu.

11 Baada yake, Eloni Mzabuloni akawa mwamuzi wa Israeli kwa muda wa miaka kumi.
12 Kisha Eloni akafa, akazikwa huko Aiyaloni katika nchi ya Zabuloni.

13 Baada yake, Abdoni mwana wa Hileli Mpirathoni akawa mwamuzi wa Israeli.
14 Naye alikuwa na wana arobaini, na wajukuu thelathini waliopanda punda sabini. Akawa mwamuzi wa Israeli kwa muda wa miaka nane.
15 Kisha Abdoni mwana wa Hileli Mpirathoni akafa, akazikwa Pirathoni huko Efraimu, katika nchi ya vilima ya Waamaleki.

# 13

*Kuzaliwa kwa Samsoni*

1 Waisraeli wakafanya maovu tena mbele za
Mwenyezi Mungu. Hivyo Mwenyezi Mungu
akawatia mikononi mwa Wafilisti kwa muda wa
miaka arobaini.
2 Palikuwa na mtu mmoja wa Sora, aliyeitwa
Manoa, wa ukoo wa Wadani, naye alikuwa na
mke aliyekuwa tasa, asiyeweza kuzaa watoto.
3 Malaika wa Mwenyezi Mungu akamtokea
huyo mwanamke na kumwambia, “Wewe ni tasa
na huna mtoto, lakini utachukua mimba na
utamzaa mtoto wa kiume.
4 Lakini ujihadhari sana usinywe divai wala
kileo kingine chochote, wala usile kitu chochote
kilicho najisi,
5 kwa kuwa utachukua mimba na utamzaa
mtoto wa kiume. Wembe usipite kwenye
kichwa chake, kwa kuwa huyo mwana atakuwa
Mnadhiri aliyetengwa kwa Mungu tangu tum-
boni mwa mama yake. Naye atawaongoza
na kuwaokoa Waisraeli kutoka mikononi mwa
Wafilisti.”
6 Ndipo huyo mwanamke akamwendea
mumewe na kumwambia, “Mtu wa Mungu
alinijia. Alionekana kama malaika wa Mungu,
wa kutisha sana. Sikumuuliza alikotoka wala
hakuniambia jina lake.
7 Lakini aliniambia, ‘Utachukua mimba na
utazaa mtoto wa kiume. Basi sasa, usinywe
divai wala kileo kingine chochote, wala usile kitu
kilicho najisi, kwa kuwa huyo mtoto atakuwa
Mnadhiri wa Mungu tangu tumboni mwa mama
yake hadi kufa kwake.’ ”

8 Ndipo Manoa akamwomba Mwenyezi Mungu,
akasema: “Ee Bwana, nakusihi huyo mtu wa
Mungu uliyemtuma kwetu aje tena, ili atu-
fundishe jinsi ya kumlea huyo mwana atakayeza-
liwa.”
9 Mungu akamsikia Manoa, naye malaika
wa Mungu akamjia tena huyo mwanamke
alipokuwa shambani; lakini mumewe Manoa
hakuwa naye.
10 Basi yule mwanamke akaenda haraka na
kumwambia mumewe, “Tazama mtu yule aliyen-
itokea siku ile yupo hapa!”
11 Manoa akainuka akaandamana na mkewe.
Alipomfikia yule mtu akamuuliza, “Je, wewe
ndiwe ulisema na mke wangu?”

Akasema, “Ni mimi.”

12 Basi Manoa akamuuliza, “Maneno yako
yatakapotimia, je, masharti ya maisha ya mtoto
huyu yatakuwa ni yapi, na kazi yake itakuwa ni
ipi?”
13 Malaika wa Mwenyezi Mungu akamjibu,
“Mke wako hana budi kufanya yale yote niliy-
omwambia.
14 Kamwe asile kitu chochote kitakachotoka
katika mzabibu, wala asinywe divai yoyote wala
kileo chochote, wala asile kitu chochote kilicho
najisi. Hana budi kufanya kila kitu nilichomwa-
giza.”
15 Manoa akamjibu yule malaika wa Mwenyezi
Mungu, “Twakuomba usubiri kwanza ili tuweze
kuandaa mwana-mbuzi kwa ajili yako.”
16 Malaika wa Mwenyezi Mungu akamjibu,
“Hata kama utanizuia, sitakula chochote kwako.

Lakini ukitaka kuandaa sadaka ya kuteketezwa, mtolee Mwenyezi Mungu.”

(Manoa hakumtambua kuwa huyu alikuwa malaika wa Mwenyezi Mungu.)

17 Kisha Manoa akamuuliza yule malaika
wa Mwenyezi Mungu, “Jina lako ni nani, ili tuweze kukupa heshima wakati maneno uliyonena yatakapotimia?”

18 Malaika wa Mwenyezi Mungu akamjibu,
“Kwa nini unauliza jina langu? Ni jina la ajabu.”

19 Ndipo Manoa akamchukua mwana-mbuzi,
pamoja na sadaka ya unga, naye akamtolea Mwenyezi Mungu dhabihu hapo juu ya mwamba. Naye yule malaika wa Mwenyezi Mungu akafanya jambo la ajabu wakati Manoa na mkewe wakiwa wanaangalia:

20 Mwali wa moto kutoka hapo madhabahuni
ulipowaka kuelekea mbinguni, malaika wa Mwenyezi Mungu akapaa ndani ya huo mwali. Manoa na mkewe, kwa kuona jambo hili, wakaanguka kifudifudi.

21 Malaika wa Mwenyezi Mungu hakumtokea
tena Manoa na mkewe. Ndipo Manoa akatambua kuwa huyo alikuwa malaika wa Mwenyezi Mungu.

22 Manoa akamwambia mkewe, “Hakika tutak-
ufa, kwa kuwa tumemwona Mungu.”

23 Lakini mkewe akamwambia, “Ikiwa
Mwenyezi Mungu alikuwa amekusudia kutuua, hangepokea sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya unga kutoka mikononi mwetu, wala hangetuonesha mambo haya yote wala kututangazia mambo haya wakati huu.”

24 Yule mwanamke akazaa mtoto wa kiume,
akamwita jina Samsoni. Kijana akakua, naye
Mwenyezi Mungu akambariki.
25 Roho wa Mwenyezi Mungu akaanza kumpa
msukumo alipokuwa huko Mahane-Dani, kati ya
Sora na Eshtaoli.

# 14

*Ndoa ya Samsoni*

1 Samsoni akateremka Timna, na huko akam-
wona mwanamke Mfilisti.
2 Alipopanda kutoka huko, akawaambia baba
yake na mama yake, "Nimemwona mwanamke
Mfilisti huko Timna; basi mnitwalie awe mke
wangu."
3 Baba yake na mama yake wakamjibu, "Je,
hakuna mwanamke miongoni mwa jamaa yako
au miongoni mwa watu wetu wote, hata ulaz-
imike kwenda kujitwalia mke kutoka kwa hao
Wafilisti wasiotahiriwa?"

Lakini Samsoni akamwambia baba yake, "Ni-
patieni huyo kwa maana ndiye alinipendeza."
4 (Baba yake na mama yake hawakujua kuwa
jambo hili limetoka kwa Mwenyezi Mungu,
kwani alikuwa akitafuta sababu ya kukabiliana
na Wafilisti; kwa kuwa wakati huo walikuwa
wakiwatawala Waisraeli.)
5 Samsoni akateremka Timna pamoja na baba
yake na mama yake. Walipofika kwenye
mashamba ya mizabibu huko Timna, ghafula
mwana simba akamjia akimngurumia.
6 Roho wa Mwenyezi Mungu akaja juu ya
Samsoni kwa nguvu, naye akampasua yule simba

kwa mikono mitupu kama ambavyo angempasua
mwana-mbuzi, wala hakumwambia baba yake
wala mama yake alichokifanya.
7 Basi akateremka na kuongea na yule
mwanamke, naye akampendeza Samsoni.
8 Baada ya muda, Samsoni aliporudi ili akam-
woe, akageuka kando ili kuutazama mzoga wa
yule simba. Tazama! Ndani ya ule mzoga akaona
kundi la nyuki na asali kiasi.
9 Akachukua asali mkononi mwake, akala huku
akitembea. Alipowafikia baba yake na mama
yake, akawapa kiasi cha ile asali, nao wakala.
Lakini hakuwaambia kuwa aliitwaa asali katika
mzoga wa simba.
10 Basi baba yake akateremka kumwona huyo
mwanamke. Samsoni akafanya karamu huko,
kama ilivyokuwa desturi ya vijana.
11 Watu walipomwona, wakaleta vijana wen-
zake thelathini ili kuwa pamoja naye.
12 Samsoni akawaambia, "Niwape kitendawili,
mkiweza kunipa jibu katika muda wa siku hizi
saba za karamu, nitawapa mavazi thelathini ya
kitani na mavazi mengine mivao thelathini.
13 Lakini msipoweza kufumbua, ndipo ninyi
mtanipa mavazi thelathini ya kitani na mavazi
mengine mivao thelathini."

Wakamwambia, "Tuambie hicho kitendawili,
hebu na tukisikie."
14 Akawaambia,

"Ndani ya mlaji,
kulitoka kitu cha kuliwa,
ndani ya mwenye nguvu,
kulitoka kitu kitamu."

Kwa muda wa siku tatu hawakuweza kutoa jibu.

15 Siku ya nne, wakamwambia mkewe Samsoni, "Mbembeleze mumeo ili atutegulie hicho kitendawili, la sivyo tutakuchoma moto wewe na wa nyumba ya baba yako. Je, mmetualika ili mpate kutunyang'anya kile tulicho nacho?"

16 Basi mke wa Samsoni akalia mbele yake na kumwambia, "Unanichukia! Hunipendi kabisa. Umewategea watu wangu kitendawili, lakini mimi hujaniambia jibu."

Samsoni akamwambia, "Tazama, sijamweleza baba yangu wala mama yangu, kwa nini nikufumbulie?"
17 Mkewe akalia kwa muda wa zile siku zote saba za karamu. Hivyo siku ya saba Samsoni akamweleza, kwa kuwa aliendelea kumsisitiza sana. Naye mkewe akawaeleza watu wake kile kitendawili.
18 Siku ya saba, kabla ya jua kutua, wanaume wa mji wakamwambia Samsoni,

"Ni nini kilicho kitamu kuliko asali?
Ni nini chenye nguvu kuliko simba?"

Samsoni akawaambia,

"Kama hamkulima na mtamba wangu,
msingekitegua kitendawili changu."

19 Ndipo Roho wa Mwenyezi Mungu akamjia Samsoni kwa nguvu. Samsoni akateremka hadi Ashkeloni, akawaua wanaume thelathini wa mji huo, akatwaa mali yao, akawapa watu wale waliotegua kile kitendawili nguo zao. Akiwa amejaa hasira, akakwea kurudi nyumbani kwa baba yake.

20 Naye mke wa Samsoni akakabidhiwa kwa
rafiki yake Samsoni aliyekuwa msaidizi wake
siku ya arusi.

# 15

*Kisasi cha Samsoni kwa Wafilisti*

1 Baada ya kitambo kidogo, wakati wa mavuno
ya ngano, Samsoni akachukua mwana-mbuzi,
kwenda kumzuru mkewe. Akasema, "Nataka
kuingia chumbani kwa mke wangu." Lakini baba
yake huyo mwanamke hakumruhusu kuingia.
2 Baba mkwe wake akamwambia, "Nilikuwa na
hakika kwamba ulimchukia, hivyo nikampeana
kwa rafiki yako. Je, dada yake mdogo si mzuri
kuliko yeye? Mchukue huyo badala yake."
3 Samsoni akawaambia, "Wakati huu, ni-
takapowadhuru Wafilisti, sitakuwa na lawama."
4 Hivyo Samsoni akaondoka na kuwakamata
mbweha mia tatu, akawafunga wawili wawili,
mikia kwa mikia. Kisha akafungia mwenge wa
moto kwenye kila jozi la mikia hiyo.
5 Akawasha ile mienge na kuwaachia wale
mbweha katika mashamba ya Wafilisti ya nafaka
zilizosimamishwa katika matita. Akateketeza
matita ya nafaka, pamoja na mashamba ya miz-
abibu na mashamba ya mizeituni.
6 Wafilisti walipouliza, "Ni nani aliyetenda
jambo hili?" Wakaambiwa, "Ni Samsoni, mk-
wewe yule Mtimna, kwa sababu mkewe ali-
peanwa kwa rafiki yake."

Hivyo Wafilisti wakapanda, wakamteketeza
kwa moto yeye huyo mwanamke pamoja na baba
yake.

7 Samsoni akawaambia, “Kwa kuwa mmetenda hivyo, hakika sitatulia hadi niwe nimelipiza kisasi juu yenu.”

8 Akawashambulia kwa ukali na kuwaua watu wengi sana. Kisha akateremka na kukaa kwenye pango katika mwamba wa Etamu.

9 Wafilisti wakapanda na kupiga kambi huko Yuda na kuenea huko Lehi.

10 Watu wa Yuda wakawauliza, “Kwa nini mmekuja kupigana nasi?”

Wakawajibu, “Tumekuja ili kumkamata Samsoni na kumtenda kama alivyotutendea.”

11 Ndipo watu elfu tatu wa Yuda waliteremka hadi kwenye pango katika mwamba wa Etamu, wakamwambia Samsoni, “Je, hujatambua kuwa Wafilisti wanatutawala? Ni nini hiki ulichotutendea?”

Akawajibu, “Nimewatendea tu kile walichonitendea.”

12 Wakamwambia, “Tumekuja kukufunga na kukutia mikononi mwa Wafilisti.”

Samsoni akawaambia, “Niapieni kuwa hamtaniua ninyi wenyewe.”

13 Wakamjibu, “Sisi hatutakuua, bali tutakufunga tu na kukutia mikononi mwao.” Basi wakamfunga kwa kamba mbili mpya na kumchukua toka huko kwenye pango katika mwamba.

14 Alipokaribia Lehi, Wafilisti wakamjia wakipiga kelele. Roho wa Mwenyezi Mungu akaja juu yake kwa nguvu. Kamba zilizomfunga mikono zikawa kama kitani iliyochomwa kwa moto, na vifungo vyake vikaanguka chini toka mikononi mwake.

15 Ndipo akaona mfupa mpya wa taya la punda,
akanyoosha mkono, akauchukua na kuua nao
Wafilisti wapatao elfu moja.
16 Ndipo Samsoni akasema,
“Kwa taya la punda
malundo juu ya lundo,
kwa taya la punda
nimeua watu elfu moja.”
17 Alipomaliza kusema, akautupa ule mfupa wa
taya; na mahali pale pakaitwa Ramath-Lehi*.
18 Kwa kuwa alihisi kiu sana, akamlilia
Mwenyezi Mungu, akisema, “Umempa mtumishi
wako ushindi huu mkuu. Je, sasa nife kwa
kiu na kuangukia mikononi mwa hawa watu
wasiotahiriwa?”
19 Ndipo Mungu akafunua shimo huko Lehi, na
maji yakatoka. Samsoni alipoyanywa maji hayo,
nguvu zikamrudia, akahuika. Hivyo chemchemi
ile ikaitwa En-Hakore†, nayo iko hadi leo huko
Lehi.
20 Samsoni akawa mwamuzi wa Waisraeli
katika siku za Wafilisti kwa muda wa miaka
ishirini.

# 16

*Samsoni na Delila*
1 Siku moja Samsoni alienda Gaza, akamwona
mwanamke kahaba, naye akaingia kwake.
2 Watu wa Gaza wakaambiwa, “Samsoni
amekuja huku!” Hivyo, wakapazingira mahali
pale, nao wakamvizia usiku kucha penye lango

---

* **15:17** maana yake *Kilima cha Taya* † **15:19** maana yake *Chemchemi ya Aliyeita*

la mji. Wakakaa kimya usiku kucha, wakiwaza, “Kutakapopambazuka, tutamuua.”
3 Samsoni akalala tu hadi usiku wa manane.
Akaamka, na kushika milango ya lango la mji, na miimo yake miwili, akaing’oa pamoja na makomeo yake. Akaviweka mabegani mwake na kuvipeleka hadi kilele cha mlima unaokabili Hebroni.
4 Baada ya hayo akampenda mwanamke
mmoja katika Bonde la Soreki aliyeitwa Delila.
5 Viongozi wa Wafilisti wakamwendea yule
mwanamke na kumwambia, “Mshawishi ili upate kujua siri ya nguvu zake zilizo nyingi na jinsi tutakavyoweza kumshinda ili tuweze kumfunga na kumtiisha. Kila mmoja wetu atakupa shekeli elfu moja na mia moja* za fedha.”
6 Hivyo Delila akamwambia Samsoni, “Naomba
uniambie siri ya hizi nguvu zako nyingi, na jinsi unavyoweza kufungwa ili kukutiisha.”
7 Samsoni akamjibu, “Kama nikifungwa kwa
kamba saba za upinde ambazo hazijakauka, hapo ndipo nitakapokuwa dhaifu kama mtu mwingine yeyote.”
8 Basi viongozi wa Wafilisti wakamletea yule
mwanamke kamba saba za upinde ambazo hazijakauka, naye akamfunga Samsoni.
9 Wakati watu wakiwa wanamvizia
katika chumba cha ndani, yule mwanamke akamwambia, “Samsoni, Wafilisti wanakujia!” Lakini yeye akazikata zile kamba za upinde, kama vile uzi wa pamba unapoguswa na moto. Hivyo siri ya nguvu zake haikujulikana.

* **16:5** Shekeli 1,100 ni sawa na kilo 13.

10 Ndipo Delila akamwambia Samsoni, “Umenifanyia mzaha na kuniambia uongo. Tafadhali niambie unaweza kufungwa kwa kitu gani?”

11 Akamwambia, “Kama nikifungwa kwa uthabiti kwa kamba mpya ambazo hazijatumika, basi nitakuwa dhaifu kama mtu mwingine yeyote.”

12 Hivyo, Delila akachukua kamba mpya na kumfunga nazo. Kisha akamwambia, “Samsoni, Wafilisti wanakujia!” Wale watu waliokuwa wanamvizia walikuwa katika chumba cha ndani. Lakini akazikata zile kamba zilizokuwa zimefunga mikono yake kama nyuzi.

13 Ndipo Delila akamwambia Samsoni, “Hata sasa umenifanyia mzaha na kuniambia uongo. Nieleze ni jinsi gani unavyoweza kufungwa.”

Samsoni akamwambia, “Kama ukivifuma hivi vishungi saba vya nywele za kichwa changu kwa nguo iliyo katika mtande, na kuukaza kwa msumari, ndipo nitakuwa dhaifu kama mtu mwingine yeyote.” Hivyo, Samsoni alipokuwa amelala, Delila akachukua vile vishungi saba vya nywele za kichwa chake na kuvifuma pamoja na nguo kwenye mtande,
14 na kuukaza kwa msumari.

Kisha akamwambia, “Samsoni, Wafilisti wanakujia!” Samsoni akaamka kutoka usingizini na kung’oa msumari na mtande, pamoja na ile nguo.

15 Ndipo Delila akamwambia, “Wawezaje kusema, ‘Nakupenda,’ wakati moyo wako haupo pamoja nami? Umenifanyia mzaha mara hizi

tatu na hujaniambia siri ya hizi nguvu zako nyingi.”

16 Hatimaye, baada ya kusumbuliwa kwa maneno kwa siku nyingi na kuudhiwa, roho yake ikataabika kiasi cha kufa.

17 Hivyo, akamwambia yule mwanamke siri yake yote, akisema, “Wembe haujapita kamwe kichwani mwangu, kwa kuwa mimi ni Mnadhiri wa Mungu tangu tumboni mwa mama yangu. Kama nywele za kichwa changu zikinyolewa, nguvu zangu zitanitoka, na nitakuwa dhaifu kama mtu mwingine yeyote!”

18 Delila alipoona kuwa amemweleza siri yake yote, akatuma ujumbe kwa viongozi wa Wafilisti na kusema, “Njooni tena mara nyingine, maana amenieleza siri yake yote.” Basi viongozi wa Wafilisti wakarudi kwa Delila, wakiwa na fedha mikononi mwao.

19 Delila akamfanya alale usingizi magotini pake, akamwita mtu amnyoe vile vishungi saba vya nywele za kichwa chake. Delila akaanza kumnyong’onyesha Samsoni, nazo nguvu zake zikamtoka.

20 Yule mwanamke akamwita, “Samsoni! Hao, Wafilisti wanakujia!”

Akaamka toka usingizini, akisema, “Nitatoka nje kama hapo awali; nitajinyoosha, niwe huru.” Lakini hakujua kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa amemwacha.

21 Basi Wafilisti wakamkamata, wakamng’oa macho yake, wakamteremsha hadi Gaza. Wakamfunga kwa pingu za shaba, wakamweka gerezani ili asage ngano.

22 Wakati huo nywele za kichwa chake
zikaanza kukua tena baada ya kunyolewa.

### *Kifo cha Samsoni*

23 Basi viongozi wa Wafilisti wakakusanyika
pamoja ili kutoa kafara kuu kwa mungu wao Dag-
oni, wakisherehekea na kusema, "Mungu wetu
amemtia adui yetu Samsoni mikononi mwetu."
24 Watu walipomwona Samsoni wakamsifu
mungu wao, wakisema:

"Sasa mungu wetu amemtia adui yetu
mikononi mwetu,
yule aliyeharibu nchi yetu
na kuwaua watu wengi miongoni mwetu."

25 Mioyo yao ilipokuwa imefurahishwa, waka-
paza sauti, wakisema, "Mleteni Samsoni aje ili
atutumbuize." Basi wakamleta Samsoni kutoka
gerezani, naye akawatumbuiza.

Wakamsimamisha katikati ya nguzo mbili.
26 Samsoni akamwambia mtumishi aliyeushika
mkono wake, "Niweke mahali ambapo ninaweza
kuzigusa nguzo ambazo zinategemeza jengo ili
nipate kuziegemea."
27 Basi lile jengo lilikuwa na wanaume na
wanawake wengi; viongozi wote wa Wafilisti wa-
likuwa humo, na kwenye dari walikuwepo watu
wapatao elfu tatu, wanaume kwa wanawake,
wakimtazama Samsoni akiwatumbuiza.
28 Ndipo Samsoni akamwomba Mwenyezi
Mungu, akasema, "Ee Bwana Mungu Mwenyezi,
unikumbuke. Ee Mungu, nakusihi ukanitie
nguvu mara hii moja tu, ili kwa tendo hili nipate

kulipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa sababu ya macho yangu mawili.”
29 Ndipo Samsoni akazikaribia zile nguzo mbili za katikati zilizokuwa zimelisimamisha lile jengo. Akazishika moja kwa mkono wa kuume, na nyingine kwa mkono wa kushoto.
30 Samsoni akasema, “Acha nife pamoja na Wafilisti!” Ndipo akazisukuma zile nguzo kwa nguvu zake zote, nalo jengo lile likaanguka juu ya viongozi na watu wote waliokuwamo ndani. Hivyo, akawaua watu wengi wakati wa kufa kwake kuliko siku za uhai wake.
31 Basi ndugu zake na jamaa yote ya baba yake wakateremka kwenda kumchukua. Wakampandisha na kumzika kati ya Sora na Eshtaoli, kwenye kaburi la Manoa baba yake. Samsoni alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka ishirini.

# 17

*Sanamu za Mika*

1 Palikuwa na mtu aliyeitwa Mika kutoka nchi ya vilima ya Efraimu.
2 Akamwambia mama yake, “Zile shekeli elfu moja na mia moja* za fedha zilizochukuliwa kwako, ambazo nilisikia ukizinenea maneno ya laana, hizi hapa; mimi ndiye niliyezichukua.”

Ndipo mama yake akamwambia, “Mwenyezi Mungu na akubariki, mwanangu.”
3 Alipozirudisha zile shekeli elfu moja na mia moja za fedha kwa mama yake, mama yake akamwambia, “Mimi nimeiweka fedha hii wakfu kwa Mwenyezi Mungu ili mwanangu atengeneze

---

* **17:2** Shekeli 1,100 ni sawa na kilo 13.

sanamu ya kuchonga, na sanamu ya kusubu. Mimi nitakurudishia wewe."
4 Hivyo akamrudishia mama yake ile fedha, naye mama yake akachukua shekeli mia mbili† za hiyo fedha na kumpa mfua fedha, ambaye aliifanyiza kinyago na sanamu. Navyo vikawekwa ndani ya nyumba ya Mika.

5 Basi Mika alikuwa na mahali pa ibada za sanamu. Akatengeneza kizibau, pamoja na miungu ya nyumbani, na kumweka mmoja wa wanawe kuwa kuhani wake.
6 Katika siku hizo, Waisraeli hawakuwa na mfalme; kila mtu alifanya alivyoona ni vyema machoni pake.

7 Palikuwa na kijana Mlawi kutoka Bethlehemu ya Yuda, aliyekuwa akiishi miongoni mwa watu wa kabila la Yuda.
8 Huyu kijana akatoka mji huo wa Bethlehemu ya Yuda na kutafuta mahali pengine pa kuishi. Alipokuwa akisafiri, akafika nyumbani kwa Mika katika nchi ya vilima ya Efraimu.

9 Mika akamuuliza, "Wewe umetoka wapi?"

Akamjibu, "Mimi ni Mlawi kutoka Bethlehemu ya Yuda, ninatafuta mahali pa kuishi."

10 Ndipo Mika akamwambia, "Ishi pamoja nami, uwe baba yangu na kuhani wangu, nami nitakupa shekeli kumi‡ za fedha kila mwaka, pamoja na nguo na chakula."
11 Hivyo yule Mlawi akakubali kuishi pamoja na Mika, naye akawa kama mmoja wa wanawe.

---

† **17:4** Shekeli 200 za fedha ni sawa na kilo 2.3 za fedha. ‡ **17:10** Shekeli 10 za fedha ni sawa na gramu 115 za fedha.

12 Basi Mika akamweka wakfu huyo kijana
Mlawi, naye huyo akawa kuhani wake na kuishi
nyumbani mwake.
13 Mika akasema, "Sasa najua Mwenyezi Mungu
atanitendea mema, kwa kuwa Mlawi huyu
amekuwa kuhani wangu."

# 18

*Wadani wahamia Laishi*

1 Katika siku hizo, Waisraeli hawakuwa na
mfalme.
Katika siku hizo, watu wa kabila la Dani
walikuwa wanatafuta mahali pao wenyewe
pa kuishi, kwa sababu walikuwa hawajafika
kwenye urithi wao miongoni mwa makabila ya
Israeli.
2 Hivyo Wadani wakatuma mashujaa watano
kutoka Sora na Eshtaoli ili kupeleleza nchi na
kuichunguza. Hawa mashujaa waliwakilisha koo
zao zote. Waliwaambia, "Nendeni mkaichunguze
hiyo nchi."
Wanaume hao wakaingia katika nchi ya vilima
ya Efraimu, wakafika nyumba ya Mika, ambako
walilala usiku huo.
3 Walipofika karibu na nyumba ya Mika,
waliitambua sauti ya yule kijana Mlawi; hivyo
wakaingia humo na kumuuliza, "Ni nani
aliyekuleta hapa? Unafanya nini mahali hapa?
Kwa nini uko hapa?"
4 Akawaeleza yale Mika aliyomtendea,
akasema, "Ameniajiri, nami ni kuhani wake."
5 Kisha wakamwambia, "Tafadhali tuulizie kwa
Mungu kama safari yetu itafanikiwa."

6 Yule kuhani akawajibu, “Nendeni kwa amani.
Safari yenu ina kibali cha Mwenyezi Mungu.”

7 Basi hao wanaume watano wakaondoka na
kufika Laishi, mahali ambapo waliwakuta watu
wanaishi salama, kama Wasidoni, kwa amani na
utulivu. Nchi yao haikupungukiwa kitu, hivyo
wakastawi. Pia walikaa mbali sana na Wasidoni,
wala hawakushughulika na mtu yeyote.

8 Waliporudi kwa ndugu zao huko Sora na Esh-
taoli, ndugu zao wakawauliza, “Mlionaje mambo
huko?”
9 Wakajibu, “Twendeni, tukawavamie! Tume-
ona kuwa nchi ni nzuri sana. Je, hamtafanya
chochote? Msisite kupanda ili kuimiliki.
10 Mtakapofika huko, mtawakuta watu walio
salama, na nchi kubwa ambayo Mungu ameitia
mikononi mwenu, isiyopungukiwa kitu chochote
duniani.”
11 Ndipo wanaume mia sita kutoka ukoo wa
Wadani, waliojifunga silaha za vita, wakaondoka
Sora na Eshtaoli.
12 Walipokuwa wakisafiri wakapiga kambi
huko Kiriath-Yearimu katika Yuda. Hii ndiyo
sababu sehemu ya magharibi ya Kiriath-Yearimu
inaitwa Mahane-Dani* hadi leo.
13 Kutoka hapo wakaenda hadi nchi ya vilima
ya Efraimu na kufika katika nyumba ya Mika.

14 Ndipo wale wanaume watano waliopeleleza
nchi ya Laishi wakawaambia ndugu zao, “Je,
mnajua kuwa katika mojawapo ya nyumba hizi
kuna kizibau, miungu ya nyumbani, sanamu ya

* **18:12** yaani *Kambi ya Dani*

kuchonga, na sanamu ya kusubu? Sasa basi, fikirini mtakalofanya.”
15 Basi wakaelekea huko, wakafika kwa yule kijana Mlawi, katika nyumba ya Mika, wakamsalimu.
16 Wale Wadani mia sita, wakiwa wamejifunga silaha, wakasimama penye ingilio la lango.
17 Wale watu watano walioenda kupeleleza nchi wakaingia ndani na kuchukua ile sanamu ya kuchonga, kile kizibau, na ile miungu ya nyumbani, na ile sanamu ya kusubu, wakati yule kuhani akiwa amesimama pale penye ingilio la lango pamoja na wale watu mia sita waliojifunga silaha.
18 Hao watu walipoingia katika nyumba ya Mika na kuchukua ile sanamu ya kuchonga, kile kizibau, na ile miungu ya nyumbani, na ile sanamu ya kusubu, yule kuhani akawauliza, “Mnafanya nini?”
19 Wakamjibu, “Nyamaza! Weka mkono wako juu ya kinywa chako na ufuatane nasi, uwe baba yetu na kuhani wetu. Si ni afadhali utumikie kabila na ukoo katika Israeli kama kuhani kuliko kumtumikia mtu mmoja na watu wa nyumbani mwake?”
20 Yule kuhani akafurahi. Akachukua kile kizibau, ile miungu ya nyumbani, na sanamu ya kuchonga, naye akaenda pamoja na wale watu.
21 Ndipo wakageuka na kuondoka, wakiwatanguliza mbele watoto wao wadogo, mifugo na mali yao.
22 Walipokuwa wamefika mbali toka nyumbani kwa Mika, watu walioishi karibu na Mika walikusanywa pamoja, nao wakawakimbiza Wadani.

23 Walipofuatilia huku wakipiga kelele, Wadani
wakageuka, wakamwambia Mika, “Una nini
wewe hata ukawaita watu waje kupigana nasi?”
24 Akawajibu, “Mmechukua miungu
niliyoitengeneza, mkamchukua kuhani wangu,
nanyi mkaondoka. Nimebaki na nini kingine?
Mnawezaje kuniuliza, ‘Una nini wewe?’ ”
25 Wadani wakamjibu, “Usibishane nasi, la
sivyo watu wenye hasira watakushambulia,
nawe na watu wa nyumbani mwako mtapoteza
maisha yenu.”
26 Basi Wadani wakaenda zao, naye Mika
alipoona kuwa wana nguvu kuliko yeye, ak-
ageuka na kurudi nyumbani mwake.
27 Kisha wakachukua vitu vile Mika alikuwa
amevitengeneza, na kuhani wake, wakaendelea
hadi Laishi, dhidi ya watu walioishi na amani
na utulivu. Wakawashambulia kwa upanga na
kuuteketeza mji wao.
28 Hapakuwa na yeyote wa kuwaokoa, kwa
kuwa waliishi mbali na Sidoni, na hawakuwa na
ushirikiano na mtu mwingine yeyote. Mji huo
ulikuwa kwenye bonde karibu na Beth-Rehobu.

Wadani wakaujenga upya huo mji na kuishi
humo.
29 Wakauita ule mji Dani kwa kufuata jina la
baba yao aliyezaliwa na Israeli, ingawa mji huo
uliitwa Laishi hapo awali.
30 Kule Wadani wakajisimamishia ile sanamu
ya kuchonga, naye Yonathani mwana wa Ger-
shomu, mwana wa Musa pamoja na wanawe
walikuwa makuhani kwa kabila la Dani hadi nchi
hiyo ilipotekwa.

31 Wakaendelea kuiabudu ile sanamu ambayo Mika alizitengeneza, wakati wote ule nyumba ya Mungu ilikuwa huko Shilo.

# 19

### *Mlawi na suria wake*

1 Katika siku hizo, Waisraeli hawakuwa na mfalme.

Basi Mlawi mmoja aliyeishi sehemu za mbali katika nchi ya vilima ya Efraimu, akamchukua suria mmoja kutoka Bethlehemu ya Yuda.

2 Lakini suria wake akafanya ukahaba, akamwacha na kurudi nyumbani mwa baba yake huko Bethlehemu ya Yuda. Baada ya kukaa huko kwa muda wa miezi minne,

3 mume wake akaenda kumsihi arudi. Alienda na mtumishi wake na punda wawili. Yule mwanamke akamkaribisha nyumbani mwa baba yake, naye baba yake alipomwona akamkaribisha kwa furaha.

4 Baba mkwe wake, yaani baba yake yule msichana, akamsihi akae. Hivyo akakaa na huyo baba mkwe wake kwa siku tatu, wakila na kunywa, na kulala huko.

5 Siku ya nne wakaamka mapema naye akajiandaa kuondoka, lakini baba wa yule msichana akamwambia mkwewe, “Ujiburudishe kwa kitu cha kula, ndipo uweze kwenda.”

6 Basi wakaketi wote wawili ili kula na kunywa pamoja. Baadaye baba wa msichana akamwambia, “Tafadhali ubakie usiku huu upate kujifurahisha.”

7 Basi yule mtu alipotaka kuondoka, baba
mkwe wake akamsihi, hivyo akabaki usiku ule.
8 Asubuhi ya siku ya tano, alipoamka ili aon-
doke, baba wa yule msichana akamwambia,
“Jiburudishe nafsi yako. Ngoja hadi alasiri!” Kwa
hiyo wote wawili wakala chakula pamoja.

9 Kisha yule mtu alipoinuka aende zake
pamoja na suria wake na mtumishi wake, baba
mkwe wake, yaani baba wa yule msichana,
akamwambia, “Tazama sasa jioni inakaribia.
Ulale hapa, usiku unakaribia. Ukae, ukajifu-
rahishe nafsi yako. Kesho unaweza kuamka
asubuhi na mapema uende nyumbani kwako.”
10 Lakini akakataa kulala tena, akaondoka na
kuelekea Yebusi (ndio Yerusalemu), akiwa na
punda wake wawili waliotandikwa, pamoja na
suria wake.
11 Alipokaribia Yebusi na usiku ukiwa
umekaribia, mtumishi akamwambia bwana
wake, “Haya sasa natuingie katika mji huu wa
Wayebusi tulale humo.”

12 Lakini bwana wake akamjibu, “Hapana.
Hatutaingia kwenye mji wa kigeni, ambao watu
wake si Waisraeli. Tutaendelea hadi Gibea.”
13 Tena akasema, “Haya, tujitahidi tufike Gibea
au Rama, nasi tutalala katika mji huo.”
14 Hivyo wakaendelea na safari, nalo jua
likazama walipokaribia Gibea ya Benyamini.
15 Wakageuka ili kuingia na kulala Gibea.
Wakaingia humo, wakaketi kwenye uwanja wa
mji, wala hakuna mtu yeyote aliyewakaribisha
kwake ili wapate kulala.

16 Jioni ile, mzee mmoja toka nchi ya vilima
ya Efraimu, aliyekuwa anaishi huko Gibea (watu
wa sehemu ile walikuwa Wabenyamini), akarudi
kutoka kwenye kazi zake za shamba.
17 Alipotazama na kuwaona hao wasafiri katika
uwanja wa mji, yule mzee akawauliza, “Ninyi
mnaenda wapi? Nanyi mmetoka wapi?”

18 Akamwambia, “Tumepita kutoka Bethle-
hemu ya Yuda, tunaelekea katika nchi ya vil-
ima ya Efraimu ninakoishi. Niliendа Bethle-
hemu ya Yuda na sasa ninaenda katika nyumba
ya Mwenyezi Mungu. Hakuna mtu yeyote
aliyenikaribisha katika nyumba yake.
19 Tunazo nyasi na chakula cha punda wetu,
pia mkate na divai kwa ajili yetu sisi watu-
mishi wako: mimi, mtumishi wako mwanamke,
pamoja na huyu kijana tuliye naye. Hatuhitaji
kitu zaidi.”
20 Yule mzee akawaambia, “Amani iwe kwenu!
Karibuni nyumbani mwangu. Nitawapa mahitaji
yenu yote, ila tu msilale katika uwanja huu.”
21 Hivyo akamwingiza nyumbani mwake na
kuwalisha punda wake. Baada ya kunawa miguu
yao, wakala na kunywa.

22 Walipokuwa wakijiburudisha, wanaume
waovu wa mji huo wakaizingira ile nyumba.
Wakagonga mlango na kusema kwa sauti kuu
kwa yule mzee mwenye nyumba, “Mtoe nje yule
mwanaume aliyeingia kwako, tupate kumlawiti.”

23 Yule mwenye nyumba akatoka nje na
kuwaambia, “Hapana, ndugu zangu, msiwe
waovu namna hii, ninawasihi. Kwa kuwa huyu

mwanaume ni mgeni wangu, msifanye jambo hili
la aibu.
24 Tazameni, hapa yupo binti yangu ambaye
ni bikira, na suria wa mtu huyu. Nitawa-
toleeni hawa sasa, mkawatwae kwa nguvu
na kuwafanyia lolote mtakalo. Lakini kwa
mwanaume huyu msimfanyie jambo ovu hivyo.”

25 Lakini wale wanaume hawakumsikiliza.
Hivyo yule mwanaume akamtoa yule suria wake
nje kwa wale watu, nao wakambaka na kum-
najisi usiku kucha hadi asubuhi. Kulipoanza
kupambazuka, wakamwachia aende.
26 Alfajiri yule mwanamke akarudi kwenye
ile nyumba bwana wake alikokuwa, akaanguka
chini mlangoni, akalala pale hata kulipopam-
bazuka.

27 Bwana wake alipoamka asubuhi na kufun-
gua mlango wa nyumba na kutoka nje ili kuen-
delea na safari yake, tazama, yule suria wake
alikuwa ameangukia penye ingilio la nyumba,
mikono yake ikiwa penye kizingiti.
28 Akamwambia yule suria, “Inuka, twende.”
Lakini hakujibu. Yule bwana akamwinua, akam-
pandisha juu ya punda wake, na wakaondoka
kwenda nyumbani.

29 Alipofika nyumbani, akachukua kisu na
kumkatakata yule suria kiungo kwa kiungo,
vipande kumi na mbili, na kuvipeleka katika
sehemu zote za Israeli.
30 Kila mtu aliyeona akasema, “Jambo la namna
hii halijaonekana wala kutendeka, tangu Wais-
raeli walipopanda kutoka Misri. Fikirini juu

ya jambo hili! Tafakarini juu ya jambo hili!
Tuambieni tufanye nini!”

# 20

### *Waisraeli wapigana na Wabenyamini*

1 Ndipo Waisraeli wote kuanzia Dani hadi Beer-
Sheba na wa kutoka nchi ya Gileadi wakatoka
kama mtu mmoja, wakakusanyika mbele za
Mwenyezi Mungu huko Mispa.
2 Viongozi wote wa makabila ya Israeli
wakakaa kwenye nafasi zao katika kusanyiko
la watu wa Mungu, ambao walikuwa askari elfu
mia nne walioenda kwa miguu wenye panga.
3 (Wabenyamini wakasikia kuwa Waisraeli
wamepanda kwenda Mispa.) Ndipo Waisraeli
wakasema, “Tuelezeni jinsi jambo hili ovu lilivy-
otendeka.”
4 Hivyo yule Mlawi, mume wa yule mwanamke
aliyeuawa, akasema, “Mimi na suria wangu tuli-
fika Gibea ya Benyamini ili tulale huko.
5 Wakati wa usiku wanaume wa Gibea wakani-
jia na kuizingira nyumba, wakitaka kuniua.
Wakambaka suria wangu hata akafa.
6 Ndipo nikamchukua suria wangu,
nikamkatakata vipande vipande na kuvipeleka
katika nchi yote ya urithi wa Israeli, kwa kuwa
wametenda uasherati mkubwa na jambo la aibu
katika Israeli.
7 Sasa, ninyi Waisraeli wote, semeni na mtoe
uamuzi wenu.”

8 Watu wote wakainuka wakasema, kama
mtu mmoja, “Hakuna hata mmoja wetu atakayeenda nyumbani. Hakuna hata mmoja wetu atakayerudi nyumbani kwake.
9 Sasa hili ndilo tutakaloitendea Gibea: Tutaikabili jinsi kura itakavyotuongoza.
10 Tutatoa watu kumi katika kila mia moja kutoka kwenye makabila yote ya Israeli, watu mia moja katika kila elfu moja, na watu elfu moja katika kila elfu kumi, ili waende wakalete mahitaji kwa ajili ya jeshi. Basi wakati jeshi litakapofika Gibea ya Benyamini, watawatendea yale wanayostahili, kwa ajili ya uovu huu walioutenda katika Israeli.”
11 Hivyo wanaume wote wa Israeli wakakutanika pamoja na kujiunga kama mtu mmoja dhidi ya huo mji.

12 Makabila ya Israeli yakatuma watu kwenda katika kabila la Benyamini lote na kuwaambia, “Ni uovu gani huu wa kutisha uliotendeka kati yenu?
13 Basi watoeni hao wanaume waovu wa Gibea, ili tupate kuwaua na kuuondoa uovu katika Israeli.”

Lakini Wabenyamini hawakuwasikia ndugu zao, Waisraeli.
14 Wakatoka katika miji yao, wakakutanika Gibea ili kupigana na Waisraeli.
15 Siku ile Wabenyamini wakakusanya watu elfu ishirini na sita kutoka miji yao waliojifunga panga, mbali na hao vijana wenye uwezo mia saba kutoka wale walioishi Gibea.

16 Miongoni mwa askari hao, palikuwa na askari mia saba waliochaguliwa waliotumia mkono wa kushoto; kila mmoja wao angetupa jiwe kwa kombeo na kulenga unywele bila kukosa.

17 Nao wanaume wa Israeli, mbali na hao wa Benyamini, wakakusanya wanaume elfu mia nne hodari wenye panga.

18 Waisraeli wakapanda Betheli na kumuuliza Mungu, "Ni nani miongoni mwetu atakayetangulia mbele yetu ili kupigana na Wabenyamini?"

Mwenyezi Mungu akawajibu, "Yuda ndiye atakayetangulia."

19 Kesho yake asubuhi, Waisraeli wakaamka na kupiga kambi karibu na Gibea.
20 Waisraeli wakaondoka ili kupigana na Wabenyamini, nao Waisraeli wakachukua nafasi zao katika vita huko Gibea.
21 Wabenyamini wakatoka Gibea na kuwaua Waisraeli elfu ishirini na mbili siku hiyo.
22 Lakini Waisraeli wakatiana moyo kila mmoja na mwenzake, nao wakachukua tena nafasi zao katika vile vita mahali pale walipokuwa siku ya kwanza.
23 Waisraeli wakapanda mbele za Mwenyezi Mungu na kulia mbele zake hadi jioni. Nao wakamuuliza Mwenyezi Mungu, "Je, tupande tena kupigana vita na Wabenyamini, ndugu zetu?"

Mwenyezi Mungu akajibu, "Pandeni mkapigane nao."

24 Ndipo Waisraeli wakawakaribia Wabenyamini siku ya pili.

25 Wakati huu, Wabenyamini walipotoka Gibea
ili kupigana na Waisraeli, wakawaua wanaume
elfu kumi na nane wenye panga.
26 Ndipo jeshi lote, na Waisraeli wote, waka-
panda Betheli, na huko wakakaa mbele za
Mwenyezi Mungu wakilia. Wakafunga siku hiyo
hadi jioni na kutoa sadaka ya kuteketezwa na
sadaka ya amani kwa Mwenyezi Mungu.
27 Nao Waisraeli wakauliza ushauri kwa
Mwenyezi Mungu. (Katika siku hizo Sanduku
la Agano la Mungu lilikuwa huko,
28 na Finehasi mwana wa Eleazari, mwana
wa Haruni, alikuwa anahudumu mbele za hilo
Sanduku.) Wakauliza, "Je, tupande tena kwenda
vitani kupigana na Wabenyamini, ndugu zetu, au
la?"

Mwenyezi Mungu akajibu, "Nendeni, kwa
kuwa kesho nitawatia mikononi mwenu."
29 Basi Waisraeli wakaweka waviziaji kuizun-
guka Gibea.
30 Kisha Waisraeli wakapanda kupigana na
Wabenyamini katika siku ya tatu na kuchukua
nafasi zao dhidi ya Gibea kama walivyokuwa
wamefanya hapo awali.
31 Wabenyamini wakatoka ili kukabiliana na
Waisraeli, ambao waliwavuta Wabenyamini
watoke katika mji. Wakaanza kupigana na
wakawaua watu wapatao thelathini wa Israeli,
kama walivyofanya nyakati nyingine, katika
uwanja na katika njia kuu, moja iendayo Betheli
na nyingine Gibea.
32 Wabenyamini walipokuwa wakiambiana,
"Wanapigwa mbele yetu kama hapo awali,"

nao Waisraeli waliambiana, “Turudini nyuma ili tuwavute wauache mji, waende kuelekea barabarani.”

33 Wanaume wote wa Israeli wakaondoka
kwenye nafasi zao na kujipanga huko Baal-Tamari, nao wale waviziaji wa Waisraeli wakatoka ghafula walipokuwa kwenye uwanda wa magharibi mwa Gibea.
34 Ndipo vijana wenye uwezo elfu kumi katika
Israeli wakaja kuishambulia Gibea. Vita vilikuwa vikali sana, hata Wabenyamini hawakutambua kuwa maangamizi yalikuwa karibu nao.
35 Mwenyezi Mungu akawashinda
Wabenyamini mbele ya Waisraeli, na siku hiyo Waisraeli wakawaua Wabenyamini elfu ishirini na tano na mia moja wenye panga.
36 Hivyo Wabenyamini wakaona kuwa
wameshindwa.

Basi Waisraeli walikuwa wamewaondokea Wabenyamini, kwa sababu Waisraeli waliwategemea hao waviziaji waliokuwa wamewaweka karibu na Gibea.
37 Wale waviziaji wakafanya haraka kuingia
Gibea, wakasambaa na kuwaua watu wote wa mji kwa upanga.
38 Waisraeli walikuwa wamekubaliana na hao
waviziaji kuwa wangesababisha wingu kubwa la moshi lipande kutoka huo mji,
39 ndipo Waisraeli wangegeuka kupigana.

Wabenyamini walikuwa wameanza kuwapiga na kuwaua Waisraeli (wapatao thelathini), hivyo wakasema, “Hakika tunawashinda kama tulivyowashinda katika vita hapo awali.”

40 Lakini nguzo ya moshi ilipoanza kupanda
kutoka mji ule, Wabenyamini wakageuka, na
tazama: katika mji mzima, moshi ulikuwa
ukipaa angani.
41 Ndipo Waisraeli wakawageukia, nao
Wabenyamini wakatiwa hofu, kwa kuwa
walitambua kwamba maafa yamewajia.
42 Basi wakakimbia mbele ya Waisraeli
kuelekea nyikani, lakini hawakuweza kukwepa
vile vita. Nao Waisraeli waliotoka katika ile miji
wakawaua huko.
43 Wakawazingira Wabenyamini pande zote,
wakawafuatia na kuwafikia karibu na Gibea
upande wa mashariki.
44 Wakaanguka Wabenyamini elfu kumi na
nane, wote wapiganaji hodari.
45 Walipogeuka na kukimbia kuelekea nyikani
hata kufikia mwamba wa Rimoni, Waisraeli
wakawaua watu elfu tano huko njiani. Wakawa-
fuatia kwa karibu hadi Gidomu, na huko
wakawaua wanaume wengine elfu mbili.
46 Siku hiyo wakawaua Wabenyamini elfu
ishirini na tano wenye panga, wapiganaji hodari.
47 Lakini watu mia sita wakakimbia kuelekea
nyikani katika mwamba wa Rimoni, na kukaa
huko muda wa miezi minne.
48 Waisraeli wakarudi na kuwaua kwa upanga
Wabenyamini wote, pamoja na wanyama na kila
walichokipata. Pia kila mji waliouona wakau-
choma kwa moto.

# 21

*Wabenyamini watafutiwa wake*

1 Wanaume wa Israeli walikuwa wameapa kiapo kule Mispa, wakasema: "Hapana mtu yeyote wetu atakayemwoza binti yake kwa Mbenyamini."

2 Watu wakaenda Betheli, wakaketi mbele za Mungu hadi jioni, wakapaza sauti zao wakilia kwa uchungu.
3 Wakasema, "Ee Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli, kwa nini jambo hili limewapata Waisraeli? Kwa nini kabila moja la Israeli limekosekana?"
4 Kesho yake asubuhi na mapema watu wakajenga madhabahu na kuleta sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani.
5 Ndipo Waisraeli wakauliza, "Ni kabila lipi la Israeli ambalo halikukusanyika mbele za Mwenyezi Mungu?" Kwa kuwa walikuwa wameapa kiapo kikuu kuwa yeyote asiyefika mbele za Mwenyezi Mungu huko Mispa, kwa hakika angeuawa.

6 Basi Waisraeli wakahuzunika kwa ajili ya ndugu zao Wabenyamini, wakasema, "Leo kabila moja limekatiliwa mbali na Israeli.
7 Sasa tutawezaje kuwapa binti zetu kuwa wake zao, hao waliobaki, na tumeapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hatutawapa binti zetu kuwa wake zao?"
8 Ndipo wakasema, "Ni kabila lipi la Israeli ambalo halikukusanyika mbele za Mwenyezi Mungu huko Mispa?" Wakagundua kuwa hakuna hata mmoja kutoka Yabesh-Gileadi aliyefika kambini kwa kusanyiko.

9 Kwa kuwa walipohesabu waliona hapakuwa
mtu yeyote wa Yabesh-Gileadi.
10 Ndipo mkutano wakatuma wapiganaji elfu
kumi na mbili, wakawaamuru kwenda Yabesh-
Gileadi na kuua kwa panga wale wote walioishi
huko, wakiwemo wake na watoto.
11 Wakasema, “Hili ndilo mtakalofanya: Ueni
kila mwanaume na kila mwanamke ambaye si
bikira.”
12 Wakapata kati ya watu walioishi Yabesh-
Gileadi wanawali mia nne, mabikira, nao
wakawachukua kwenye kambi huko Shilo katika
nchi ya Kanaani.
13 Ndipo mkutano ukatuma ujumbe wa amani
kwa Wabenyamini huko katika mwamba wa
Rimoni.
14 Basi Wabenyamini wakarudi wakati ule,
nao wakapewa wale wanawali wa Yabesh-
Gileadi waliohifadhiwa. Lakini hawakuwatosha
wanaume wote.
15 Waisraeli wakahuzunika kwa ajili ya
Wabenyamini, kwa kuwa Mwenyezi Mungu
alikuwa ameweka ufa katika makabila ya Israeli.
16 Viongozi wa kusanyiko wakasema,
“Kwa kuwa wanawake wa Wabenyamini
wameangamizwa, tufanyeje ili kuwapatia wake
wale wanaume waliosalia?”
17 Wakaendelea kusema, “Lazima tuwape
Wabenyamini waliopona wake ili wawe na
warithi, nalo kabila lolote katika Israeli lisifutike.
18 Hatuwezi kuwapa binti zetu kuwa wake,
kwa kuwa sisi Waisraeli tumeapa kiapo hiki:
‘Alaaniwe mtu yeyote ampaye Mbenyamini
mke.’ ”

19 Ndipo waliposema, “Tazama iko sikukuu ya
kila mwaka ya Mwenyezi Mungu katika Shilo,
kaskazini mwa Betheli na mashariki mwa ile
barabara inayotoka Betheli kwenda Shekemu,
upande wa kusini wa Lebona.”
20 Hivyo wakawaelekeza Wabenyamini,
wakisema, “Nendeni mkajifiche kwenye
mashamba ya mizabibu,
21 na mkae macho. Wasichana wa Shilo
watakapojiunga kwenye kucheza, tokeni kwenye
hayo mashamba ya mizabibu, na kila mmoja
ajinyakulie mke kutoka miongoni mwa hao wa-
sichana wa Shilo, nanyi mwende nao katika nchi
ya Benyamini.
22 Baba zao au ndugu zao watakapotu-
lalamikia, tutawaambia, ‘Kuweni wakarimu
kwetu, nanyi mturuhusu tuwe nao kwa kuwa
hatukuweza kumpa kila mtu mke tulipopigana.
Lakini ninyi pia hamna hatia, kwa kuwa
hamkuwapa wao binti zenu kuwa wake.’ ”
23 Basi hivyo ndivyo Wabenyamini walivy-
ofanya. Wasichana walipokuwa wakicheza, kila
mtu akanyakua msichana mmoja, akaenda naye
ili awe mke wake. Kisha wakarudi katika urithi
wao na kuijenga upya miji na kuishi humo.
24 Wakati huo Waisraeli wakaondoka sehemu
ile na kwenda nyumbani kwao, kwa makabila
yao na kwa jamaa zao, kila mmoja kwenye urithi
wake mwenyewe.
25 Katika siku hizo, Waisraeli hawakuwa na
mfalme; kila mtu alifanya alivyoona ni vyema
machoni pake.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d